MKUTANO WA TANO

Kikao cha Tisa – Tarehe 25 Oktoba, 2011

(Kikao kilianza saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 10

Kupungua kwa Idadi ya Wapiga Kura Katika Uchaguzi wa Mwaka 2010

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:-

Katika Uchaguzi Mkuu uliopita wa mwaka 2010, takwimu ilionesha kuwa idadi ya wapiga kura ilikuwa ndogo ikilinganishwa na ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 hali ambayo ni yenye kutatanisha.

(a) Je, ni idadi gani ya wapiga kura iliyopungua kwa kulinganisha chaguzi za awamu hizi mbili.

(b) Ni chombo gani/taasisi gani iliyohusika na tokeo hilo.

(c) Serikali imejifunza nini kutokana na tokeo hilo.

(d) Serikali imejiandaa vipi katika kurekebisha hali hiyo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 10 lenye kifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, idadi ya wapiga kura waliojiandikisha kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 walikuwa ni 507,225 na wapiga kura waliojitokeza kujiandikisha kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 walikuwa ni 407, 658. Kulikuwa na tofauti ya wapiga kura 99,567.

(b) Mhe. Spika, hakuna taasisi hata moja ya kulaumiwa kuhusu matokeo hayo. Kupanda na kushuka idadi ya wapiga kura kunategemea na mambo mengine ya

mwamko wa wapiga kura wenyewe. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ambayo kwa mujibu wa sheria ndiyo yenye mamlaka ya kuandikisha wapiga kura, kwa kipindi cha zaidi ya miezi tisa (Julai 2009 mpaka Mei, 2010) katika awamu mbili tofauti ilipita katika kila Shehia Unguja na Pemba kuandikisha wapiga kura wapya na kurekebisha taarifa za wapiga kura wa zamani na idadi ya wapiga kura iliyoelezwa katika jawabu la kifungu cha (a) ndiyo pekee iliyojitokeza katika zoezi hilo la Tume.

(c) Mhe. Spika, kwa toleo hilo Serikali imejifunza mambo matatu makuu yatuatayo:-

- Kwamba idadi ndogo ya wapiga kura ndio ambao waliojitokeza katika zoezi la tume ya Uchaguzi la matayarisho ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, ikilinganishwa na idadi ya wapiga kura waliojitokeza katika mwaka 2005.

- Kwamba ipo haja kubwa ya kuimarisha kwa shughuli za utoaji wa elimu ya wapiga kura ili kila mwenye haki ya kupiga kura ashiriki kikamilifu katika shughuli za uchaguzi.

- Kuchukua kila hatua ya kurekebisha kasoro ndogo ndogo zinazojitokeza katika mchakato mzima wa zoezi la uchaguzi Mkuu.

(d) Mhe. Spika, kwa kuanza na mwaka wa Fedha 2011 – 2012 na kwa kuwa shughuli za Tume ya Uchaguzi ni endelevu kutokana na kuwepo kwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Serikali itakuwa ikitenga fedha kwa Tume ya Uchaguzi kuiwezesha kutoa elimu ya wapiga kura kwa kipindi chote hata baada ya uchaguzi ili kuwaelimisha wapiga kura juu ya haki zao za msingi za kupiga kura.

Aidha serikali inaendelea na jitihada zake za kurekebisha kasoro ndogo ndogo zinazojitokeza katika uchaguzi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Katika takwimu zilivyo idadi ya watu Zanzibar inaongezeka kila siku na Mwenyezi Mungu tunamshukuru na atujaalie hivyo hivyo hakujatokea janga lolote lililosababisha upungufu wa watu, katika kujiandikisha kuna mambo lazima mtu atimize ndio apate kujiandikisha nauliza suala hili nikiwa tayari watu wengi wamo katika daftari la kujiandikisha.

a) Kwanza atimize umri na katika katiba inaeleza mtu apelike kielelezo chachote kinachotimia umri wake, lakini wapiga kura wetu waliokuwa na vyeti vya kuzaliwa na kwa sababu sina *register* na vinatambulika hakika kuwa ni vyeti vyao wenyewe kwa vielelezo vyote Sheha alikuwa anavikataa, alisema ni lazima upate cheti cha *register* na kupata cheti hiyo Pemba hakuna usumbufu ni mkubwa mpaka watu weje Unguja na kundi lote lile la watu

hawakuandikishwa wakati wanavyo vyeti vya kuzaliwa, sababu ni kuwa haviku-*register* tu mbali wengine waliokuwa na vielelezo vyengine.

b) Kuna watu siku zote hizo walikuwa wakipiga kura zote lakini safari hii kwa sababu ya kutokuwa na kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi wakaambiwa safari hii hawapigi.

Swali langu ni hivi;

i) Nikiona hivi ni moja katika sababu kuu zilizosababisha watu kupungua hivyo kama Mhe. Waziri moja kwa moja kama alivyonijibu nataka nijue ni kwa sababu gani hasa ikawa ni lazima kupatikane cheti cha kuzaliwa cha *register* ndio mtu aweze kuandikishwa kuwa mpiga kura.

ii) Kwa nini watu wote wakanyimwa na wengine ni wenye umri zaidi kuliko mie walikuwa wakipiga kura na vielelezo vyao wanavyo, safari hii wakakataliwa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Sina hakika kama nimemfahamu vizuri Mjumbe kwa sababu amezungumza sana na haraka haraka, lakini kwa kadiri nilivyomfahamu nitajibu swali kwa nilivyolifahamu.

Mhe. Spika, baada ya uchaguzi wa mwaka 2005 palitungwa sheria mbili au palirekebishwa sheria mbili. Moja ni sheria ya kujiandikisha ilifanyiwa marekebisho na pili ikatungwa sheria ya ukaazi, kwa hivyo kuhitaji mpiga kura aje na shahada mbili moja ya ukaazi na moja ya Uzanzibari suala hilo lilifanywa kwa mujibu wa sheria.

Kutokana na uchaguzi wa mwaka 2005 kwa kuwa kipindi hicho kulikuwa na kitambulisho cha kupiga kura tu peke yake ndipo idadi ikawa kubwa kwa sababu yumkin wapo ambao sio Wazanzibari lakini kwa sababu walikuwa na kitambulisho cha kupiga kura walipata nafasi ya kupiga kura, tabaan idadi hiyo ikawa kubwa. Lakini baada ya kuja ile sheria kwamba nakitambulisho cha Mzanzibari lazima uwe nacho uwe na vitambulisho viwili cha kwanza cha kupiga kura cha kujiandikisha lakini cha pili cha Uzanzibari, ndipo watu wengi wakashindwa kwenda kujirekebisha na kujiandikisha katika mwaka 2010 na matokeo yake hadi hivi leo ninapozungumza kuna vitambulisho vya kupiga kura 7,324 bado havina wenyewe.

Vitambulisho hivyo vilitumika kupigia kura mwaka 2005, kutokana na hali hiyo na hiyo ni sababu ya msingi iliyopelekea kupungua idadi ya wapiga kura mwaka 2010.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Katika suala langu nilisema wako Wazanzibari ambao wana sifa ya kuandikishwa kwa kutimia umri na wana vyeti vya kuzaliwa lakini *sio register* na katika katiba wala kwenye hizo sheria za uchaguzi, haikusema kwamba lazima kuwe cheti *register*. Kwa nini wale wakaachwa.

Lakini huwezi kupata cheti cha Mzanzibari ukaazi bila ya kupata barua kutoka kwa Sheha na sheha kama huna cheti cha *register* hakupi, sasa tuangalie mazingira ya Zanzibar na jambo hili limetokezea juzi tushafanya mazoezi huko nyuma, ilikuwa kuna sababu gani hata wale waliokwisha kupiga kura na wanajulikana kwamba umri wao ni mkubwa, kwa sababu wasingeliruhusiwa kupiga kura na safari hii wakaachiwa kwa sababu hawana cheti cha kuzaliwa *register.*

Suala hilo hakuligusa kwa upande huu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Suala la kwenda kujiandikisha Uzanzibari linaambatana na sheria ya Mzanzibari iliyopo pamoja na maelezo katika katiba, unapokwenda kujiandikisha kama ni Mzanzibari kwanza unatakiwa ujulikane hapo unapoishi ndipo unapoishi na ndipo ulipotaka kupigia kura, kwa hivyo maelezo ya sheha ni muhimu kupatikana karatasi ya kuzaliwa hali kadhalika ni muhimu kupatikana ili ijulikane kwamba mtu huyu amefikia umri wa kupiga kura, vitu hivyo viwili uthibitisho wa sheha na karatasi ya kuzaliwa ikipatikana unakwenda kujiandikisha kama ni Mzanzibari na ukifika wakati kama kwenda kujiandikisha kwenye daftari unakwenda kujiandikisha.

Lakini kama kumetokea kasoro za aina hiyo hayo ndio marekebisho tunayosema katika jibu nitakalokuja kukujibu baadae ndio yatakayofanywa

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza lenye sehemu a na b.

Jana tume ya Uchaguzi wakati inawasilisha ripoti yake ya uchaguzi uliopita ilisema kwamba inapendekeza watu waliopo mahospitali wagonjwa pamoja na walioko mahabusu waruhusiwe sasa kupita kura.

a) Kwa hivyo kufuatia sasa maelekezo hayo ya tume. Je, Serikali haioni haja kwamba Wazanzibari wote walioko nje ya nchi sasa wakati umefika ili nao waruhusiwe kupiga kura.

b) Kwa kuwa sasa tunaongozwa na serikali ya JNU je, kufuatia *sprit* hiyo iliyopo sasa ya kuwa na serikali ya umoja wa kitaita. Serikali haioni haja ya kubadili sheria ili kulegeza masharti yaliyomo kwenye sheria ili kuwawezesha Wazanzibari wengi kupata haki yao ya msingi ya kuchagua viongozi wao.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Serikali italiangalia suala la mahaburu kupata haki ya kupiga kura, kwa kufuata hivyo itabidi sheria irekebishwe na kama serikali itaona kuna haja hiyo sioni sababu ya kulizuia hilo, lakini kama serikali itaona mahabusu aliyetimiza miezi sita jela kwa mujibu wa sheria hataruhusika kupiga kura na ikiona kwamba kuna haja hiyo kutakuwa hakuna haja ya kurekebisha sheria, kwa hivyo mahabusu watakuwa hawapati kupiga kura.

Lakini mahabusu ambao wamekaa muda mdogo pale katika jela au katika Chuo cha Mafunzo na kama serikali itaona kuna haja ya kurekebisha sheria, sheria itabadilishwa na mahabusu watapata haki ya kupiga kura.

Suala la pili linahusu watu walioko nje ya nchi waruhusiwe kupiga kura, nalo hilo ni suala la maamuzi ya pamoja ya serikali kama serikali itaona kuna haja hiyo ile sheria ya makaazi ya pahala katika eneo unalopiga kura ya miezi kadhaa itakuwa inaondolewa, na hao watapata haki ya kupiga kura.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa maji hupatikana katika visima kwenye maeneo mbali mbali, lakini serikali huona haja ya kuagiza mashine na kuweka mamlaka ya maji ili kuwafikishia wananchi majumbani.

Je, hili suala la vitambulisho vya Mzanzibari haioni haja ya kuwapunguzia ufumbufu wananchi kwa kuwapatia vitambulisho kwa wakati, hasa wanafunzi ambao ni wetu wenyewe wako maskulini lakini mpaka wamelize Form IV hajakionja kitambulisho hicho.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Hata nami alipoanzia suala la visima na maji nikaona labda kababaika kuona mimi nipo hapa lakini baada ya kuendelea na maelezo yake nikamfahamu alikusudia kusema nini.

Ni kweli kama mwanafunzi aliyeko skuli na ametimiza miaka kumi na nane (18) ana haki ya kupata kitambulisho cha Mzanzibari, sasa shughuli za kutoa vitambulisho vya Uzanzibari au vya ukaazi ni shughuli inayoendelea kila siku, katika skuli zozote kuna lile eneo la *holy days* ambazo Mwanafunzi anakuwa nje ya skuli na anapata nafasi nzuri sana ya kufanya mambo yake mengine. Sasa kama mwanafunzi huyo angekwenda sehemu ya vitambulisho akaomba kitambulisho akakikosa eti kwa sababu ni mwanafunzi tu hilo nadhani lingekuwa ni kosa kubwa.

Lakini kama mwanafunzi aliyetimiza umri na anakwenda kutafuta kitambulisho, kitambulisho hicho mwanafunzi ana haki ya kupewa.

Nam. 88

Utaratibu wa Meli Kupakia Mizigo na Abiria

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Zanzibar ni Visiwa na kwa sehemu kubwa maisha ya wananchi wake hutegemea sana usafiri wa vyombo vya baharini, zikiwemo meli.

(a) Ili meli iweze kubeba mizigo na abiria hutakiwa iwe na sifa gani.

(b) Katika hatua ya meli inapoanza kupakia abiria na mizigo hadi inapoondoka ni vyombo vingapi vya dola (Serikali) vinavyopaswa kushughulikia zoezi hilo.

(c) Ni nani mwenye amri ya mwisho ya kuiruhusu ama kutoiruhusu meli kuondoka.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam 88 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo;

(a) Ili meli iweze kubeba abiria na mizigo ni lazima iwe imeundwa kufanya hivyo yaani iwe na sehemu ya kukaa abiria na sehemu ya kuwekea mizigo. Aidha iwe na vifaa vya kuzimia moto na vifaa vya kuokolea maisha kwa idadi isioyopungua ya idadi ya watu iliyoruhusiwa kuchukua. Halikadhalika iwepo "stability booklet" itakayoeleza kuwa Meli hiyo inauwezo wa kuchukua idadi kadha ya abiria na mizigo.

(b) Meli inapopakia abiria hadi kuondoka katika maeneo ya bandari kuna vyombo kadhaa ya dola (Serikali) ambavyo vinasimamia zoezi zima ya upandaji wa abiria chomboni. Vyombo hivyo ni Mamlaka ya kusimamia Usafiri wa Baharini, Shirika la Bandari, Bodi ya Mapato (ZRB) na vyombo vya Ulinzi kama vile Polisi, Usalama wa Taifa na KMKM.

(c) Mwenye amri ya mwisho ya kuiruhusu ama kutoiruhusu chombo kuondoka bandarini ni Mamlaka ya Usafiri wa Baharini kwa kushirikiana na Taasisi husika zinazosimamia upakizi wa abiria. Hata hivyo uwezo huu haukatazi Mamlaka nyengine kuzuia meli kuondoka bandarini kwa malengo ya kulinda usalama wa wananchi wetu na nchi yetu kwa jumla.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize kama ifuatavyo kifungu a, b na c.

Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba ili meli iweze kuondoka basi kuna vyombovingi ambavyo kwa kushirikiana vinafanya kazi hiyo ya kuruhusu meli kuondoka. Hivi karibuni mamlaka yake imezuia baadhi ya vyombo kusafiri baharini kwa visingizio tofauti ikiwemo ubora wa meli hizo, jambo ambalo huko nyuma meli hizo hizo zimefanya kazi hiyo hiyo zaidi ya miaka kumi.

a) Naomba kujua utaalam huo wa kujua juzi hapo nyuma ulikuwa haupo.
b) Kwa kuwa vyombo zaidi ya vitano vinapaswa kushirikiana na suala hilo na kwa kuwa meli zinaondoka kwa kukiuka utaratibu. Je, anakusudia kunambia kwamba watendaji hawa hawana sifa za kupewa dhamana hizi.
c) Amesema kwamba matakwa hayo ya kisheria hayafanyi meli isiondoke ninavyojua mimi anayeruhusu kuingia na kuondoka meli kuondoka ni

wataalam wa *signal tower*. Anakusudia kuniambia kwamba mnara huo sasa hauna maana.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:

a) Ni kweli mamlaka husika ya usafiri wa baharini (ZMA) ilivizuia vyombo hivyo na ilivizuia kwa mujibu wa sheria na taratibu inavyowaruhusu na walifanya hivyo baada ya kujiridhisha. Mamlaka ya (ZMA) ina uwezo wa kuchunguza chombo chochote cha baharini na watakapogundua kwamba chombo hicho kina mapungufu wana mamlaka ya kisheria kuweza kukizuia na hali hiyo ndio iliyotokezea. Baada ya kuvichunguza na kugundua kwamba kuna kasoro hadi hapo watakapoonyesha kasoro hizo wataweza kuziruhusu kuendelea na safari zao.

b) Mhe. Spika, meli yoyote itakayoondoka inatakiwa ifuate utaratibu kwa kuruhusiwa na vyombo vinavyohusika kama tulivyotaja katika majibu mama, kama kitatokezea chombo kitaondoka bila ya utaratibu au kinyume Mamlaka husika kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bandari tuna utaratibu za kuvizuria vyombo hivyo hata vikiwa viko safarini na kuvitaka visimame na virudi katika bandari yetu.

   Naamini kwamba hakujakuwa na mapindukio ya mara kwa mara ya ukiukwaji wa taratibu hizi kwa vyombo kuondoka bila ya kufuata utaratibu wa Mamlaka husika.

c) Suala la Mheshimiwa Muwakilishi alichokiuliza ni chombo gani chenye mamlaka ya kuruhusu meli kuondoka au kutokuondoka, tulichomjibu ni Mamlaka ya Usafiri baharini ndio chombo chenye mamlaka ya kuruhusu aidha meli kuondoka au kutokundoka, sio vyombo vinavyoelekeza muda gani wa kufunga au pahali gani. Chombo chenye mamlaka ni (ZMA)

Nam. 89

Ukodishaji wa MV Ukombozi

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa Wazanzibari wamekuwa wakisikia kukodishwa kwa Meli ya MV Ukombozi kwa Kampuni ya GAPCO.

(a) Je, meli hiyo imekodishwa kwa thamani na muda gani.

(b) Fedha zinazolipwa huingia katika mfuko gani.

(c) Je, upo mkataba uliohusika na ukodishwa wa meli hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mwakilishi, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifutavyo.

Mhe. Spika, meli ya MT. Ukombozi ni meli ya kubebea mafuta meli hiyo imeundwa miaka ya thamanini (1980) nchini Japan. Uwezo wake ni kubeba tani 2,000 kwa wakati mmoja aidha meli hiyo imeundwa kwa kuwa na mkuku mmoja *single hall*. Kwa muda mrefu meli hiyo imekuwa ikifanya safari zake kwa kubeba bidhaa za mafuta ya serikali na baadae ikaanza kubeba mafuta ya kampuni ya mafuta ya *ECOTEC* kwa muda wote huu meli hiyo iko salama na inaendelea na safari zake vizuri, zaidi ya zile safari ya kwenda chelezoni kwa mujibu wa sheria za usafiri wa baharini zinavyoelekeza.

Mhe. Spika, baada ya kampuni ya *ECOTEC* kuondoka katika soko la bidhaa ya mafuta hapa Zanzibar meli hiyo ilirejeshwa katika dhamana za uendeshaji wa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar, baada ya hapo kampuni husika ya mafuta ya *CAPCO Company LTD* ilijitokeza na kuonyesha dhamira ya kuikodi meli hiyo. Shirika letu la Meli na Uwakala limeingia mkataba na kampuni hiyo na kuikodisha, hivyo basi meli hiyo hadi wakati huu imekodishwa kwa kampuni ya *CAPCO.*

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:

(a) Meli hiyo imekodishwa kwa CAPCO kwa dola 3,335 kwa siku, muda wa mkataba ni mwaka mmoja kwa ruhusa za pande zote mbili unaweza kuendelea mkataba huo, aidha mkataba huu ni kuimarika kutokana na mkataba wa awali ambapo serikali ilikuwa ikilipwa dola 2,900 kwa siku

(b) Shirika la Meli na Uwakala ni shirika linalojitegemea hivyo mapato yake yote ikiwemo fedha za kodi hiyo ya MT. Ukombizi kwa kila mwezi huingizwa katika mfuko wake mkuu wa shirika husika.

(c) Kama tulivyoeleza kwamba meli hiyo imekodishwa kwa kampuni binafsi na mikataba hiyo ipo na imefuata taratibu zote husika kwa mujibu wa sheria husika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza lenye vifungu a na b kama ifuatavyo:

Mahesabu ambayo Mhe. Naibu Waziri alitupa ni zaidi ya bilioni mbili kwa mwaka na Zanzibar tuna tatizo kubwa sana la vyombo vya uhakika kwa ajili ya wananchi wetu, kwa kuwa Wizara hii hii imewahi kuuza Meli ya MV. Mapinduzi kwa dola laki nne na kumi (4,010,000) na kwa kuwa Shirika la Meli ni Shirika la Umma ambalo linalea wafanya biashara.

a) Ni sababu zipi za msingi ambazo serikali kwa mapato yote haya inashindwa kuhudumia Wazanzibari kwa kununua meli mpya ya kisasa ambapo Wazanzibari wanateseka.

b) Zipo shtuma kwamba Shirika la Meli na Uwakala kazi kubwa wanayoifanya ni kutafuna fedha za umma, hili anasemaje?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, Meli ya MV. Ukombozi imekodishwa kwa kampuni ya *CAPCO* kutoka nyuma hadi mwezi Septemba mwaka huu ulipoisha mkataba walikuwa wanatulipa dola 2,900 kwa siku.

(a) Ni kweli kwa hisabu za haraka utaona ni fedha nyingi. Lakini mkataba tulioingia nao ni mkataba wa kila mwaka na malipo haya anatulipa kwa mwezi na utaratibu wa mkataba wetu ni kwamba meli ile katika shughuli za uendeshaji, ukiachilia mbali mafuta ambayo wana-*operate* wao wenyewe, gharama nyengine zote zinatakiwa kuendeshwa na shirika letu.

Kwa hivyo, fedha zile ambazo wanatulipa tunatakiwa tutowe sehemu ya kuendeshea meli hiyo. Naamini kwamba hicho kiwango cha bilioni 2 anazofikiria Mhe. Hija Hassan hakitotimia baada ya kuchukua huo uendeshaji na gharama nyengine zinazoendeshwa na shirika. Natambua umuhimu, haja na ulazima wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwa na meli. Jambo hili tayari nimeshalieleza, dhamira na mikakati ya serikali katika kufanikisha jambo hilo.

Niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi, muendelee kuwa na subira, serikali hii sikivu, ina mapenzi na wananchi wake na imedhamiria kupata ufumbuzi wa tatizo hili.

(b) Mhe. Spika, Shirika la Meli na Uwakala ni chombo kilicho chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Malengo na madhumuni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuona uadilifu, uaminifu, ukweli wa mashirika na watendaji wake. Kama Mhe. Spika, itathibitika kwamba shirika hili halitendi hivyo, yaani linakwenda kinyume na maelekezo ya serikali basi naamini serikali itachukua hatua stahiki kwa wale wahusika.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kwa kuwa Meli ya MV Ukombozi ni mali ya serikali, napenda kumuuliza Mhe. Waziri kwamba

(a) Je, mara ya mwisho ya ukodishwaji wa meli hii ni makampuni mangapi yaliyojitokeza katika kutaka kuikodi meli hiyo.

(b) Kwa kuwa meli hii imechakaa sana kama alivyoeleza Mhe. Waziri na kwa kuwa serikali ina utaratibu wa kuuza mali chakavu. Kwa nini serikali haifikirii kuiuza meli hii ili ikapata fedha kwa ajili ya kununua meli mpya, pamoja na

kuepuka hasara ya kuzama meli hii katika mikono ya serikali ya serikali kama ilivyotokea kwa MV Mapinduzi, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, katika majibu mama nilieleza kwamba meli hii asili yake ilikuwa ikifanyiwa kazi ya kubeba bidhaa ya mafuta wakati huo ikiwa chini ya serikali.

(a) Baadae baada ya kuja kampuni ya *ECOTEC* meli hii ikakodishwa katika kampuni ya *ECOTEC*. Kwa muda huu kampuni ambayo imekodishwa ni kampuni ya *GAPCO*. Ni dhahiri wazi kwamba ili tuweze kuifanya biashara hiyo, tunahitaji kampuni ambayo itakuwa na uwezo mkubwa wa kufanya huduma hiyo ya mafuta. Kwa muda huu kampuni ambayo imechukua soko la mafuta Zanzibar ni kampuni ya *GAPCO.*

Hali hiyo ndio iliyopelekea kampuni hii kujitokeza peke yake pasi na kupata mshindani wa kuja kuomba kukodi meli hii, kwa kutambua tu kwamba hao wengine hawana uwezo wa kufanya biashara kiasi hicho cha kuweza kuagiza mafuta kwa njia ya meli. Wengi wa makampuni hayo wanachukua mafuta kutoka kwake yeye akiwa ndio *man supply* wa huduma hiyo ya mafuta hapa nchini.

(b) Mhe. Spika, meli hii kama tulivyoeleza kwamba imetengenezwa miaka ya 1980, na kitaalamu meli hii ina mkuku mmoja. Kwa mujibu wa taratibu za IMO, meli hii uwezekano wake wa kutumika ni hadi mwaka 2013. Naamini kwamba ni vyema kutaka kuiuza, lakini naamini kwamba hilo soko halitokuwepo. Ni busara kwetu sisi wenyewe tukaendelea kuitumia hadi hapo muda utakapofika, ili tuweze kufanya maamuzi ya kuweza kuona yatakayoleta tija na maslahi na kuweza kutumia huduma zetu za ndani.

Mhe. Spika, naamini kama atatokea mtu anahitaji meli hii kwa kiwango ambacho serikali itaridhika na kuona kitakuwa na tija, basi serikali haitokwama. Lakini kama itakuwa kwa jambo ambalo litapelekea kuleta usumbufu mkubwa zaidi kwa serikali na wananchi wake, sidhani kama serikali itafikia maamuzi hayo.

Mhe. Spika: Majibu ya maswali haya yamechukua muda mrefu kidogo, kwa hivyo tukomee hapa. Mhe. Naibu Waziri tunakushukuru. Waheshimiwa Wajumbe, niwaombe radhi kidogo kuingilia kipindi hiki cha maswali. Tumepata ugeni ambao ni ujumbe wa Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, wamefika hapa kwa ajili ya kutoa mkono wa rambirambi, kutokana na msiba mkubwa ambao umetufika hivi karibuni kwenye mwezi wa Septemba.

Kwa hivyo, kama kawaida sisi wote ni Watanzania, msiba ule ulikuwa ni wa kitaifa, hivyo ni msiba wa Watanzania wote. Kwa hivyo, wameona jambo lile lisipite hivi hivi bila ya kuja kutujulia hali na kutoa mkono wa rambirambi kupitia kwa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Kwa bahati nzuri walikutana katika ofisi yake ya hapa katika jengo hili la Baraza la Wawakilishi. Basi nichukuwe nafasi hii ili kuwatambua wageni wetu waliofika ambao wanaongozwa na Mhe. Mkuu wa Mkoa nao ni hawa wafuatao.

Mhe. Leonidas Gama Mkuu wa Mkoa, Mhe. Anna Nyambi huyu ni Mkuu wa Wilaya ya Siha, Mhe. Mussa Samizi Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Mhe. Noman Sigala Mkuu wa Wilaya ya Hai, Mhe. Mena Swai Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika NCU na Mr. Gobles Kimaro *Deputy Private Sector* wa Mkuu wa Mkoa.

Mhe. Mkuu wa Mkoa na ujumbe wako karibuni sana, tunawashukuru sana kwa kuja kutupa mkono wa rambirambi, kutokana na msiba mkubwa uliotufika kwa Watanzania wote na tunawakaribisha sana katika jengo la ukumbi wetu huu wa Baraza la Wawakilishi na kupata nafasi ya kushirikiana na sisi leo asubuhi, hasa katika kipindi hiki cha Maswali na Majibu.

Kwa hivyo, niwaombeni basi baada ya shughuli hii ya kutoa mkono wa rambirambi kwetu, mrudi salama nyumbani bila ya matatizo yoyote, karibuni sana na ahsanteni sana. Tunaendelea.

Nam. 68

Huduma ya Maji Safi, Jimbo la Mpendae

Mhe. Mohammed Said Mohammed – Aliuliza:-

Kwa kuwa viongozi wa Jimbo la Mpendae wamefanya jitihada kubwa ya kuwaletea maji wananchi wao kwa kuchimba visima na kununua mashine kuwa mpya, lakini kutokana na *line* hizo kuwa za zamani, imekuwa ni kikwazo kwa wananchi wetu kupata maji safi kutokana na uchakavu wa *line* hizo.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kuunga mkono jitihada za viongozi hao wa jimbo, ili kuondosha tatizo la ukosefu wa maji safi jimboni hapo.

(b) Ili kukomesha tatizo la ukosefu wa maji safi na salama, ni lini serikali itaanza kusambaza *line* mpya (mfumo huu mpya) wa maji katika Jimbo la Mpendae.

(c) Je, serikali haioni kuwa kuendelea kukosekana maji safi na salama kunarudisha nyumba azma ya Mapinduzi matukufu ya 1964 na pia huwakosesha imani na mapenzi wananchi wetu kwa serikali yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 68 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara yangu kwa kupitia Mamlaka ya Maji, itaendelea kushirikiana na viongozi hao kama tulivyochukua hatua za uchimbaji wa kisima hicho na kulaza mabomba makubwa kutoka katika kisima hicho na kuwafikia wananchi.

(b) Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika jibu (a) wizara yangu itaendelea na jitihada za kulaza mabomba madogo, kwa kuunganisha na mtandao wa mabomba makubwa yatakayowawezesha wananchi wa maeneo hayo kupata huduma ya maji safi na salama.

(c) Mhe. Spika, kwa kutambua hayo ndio maana wizara yangu iliamua kwa makusudi kuanzisha mradi wa kuchimba visima, kulaza mabomba, kulaza mabomba makubwa na itaendelea na kuchukua hatua za kulaza mabomba madogo madogo yaendayo kwa wananchi, katika dhana nzima ya kuyalinda, kuyatunza na kuyaenzi Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964 yaliyomkomboa Mzanzibari.

Nam. 71

Nyumba ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Iliyopo Welezo

Mhe. Mohammed Said Mohammed – Aliuliza:-

Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati iliwahi kukata viwanja kwa ajili ya makaazi ya watu eneo la Welezo karibu na kambi ya Jeshi la Wananchi la Tanzania (JWTZ) na baadae kuvigawa kwa wananchi. Mmoja kati ya watu waliopata viwanja katika eneo hilo na kujenga nyumba ni Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Mhe. Abdalla Mwinyi Khamis. Hata hivyo, baadae serikali ikaamuru sehemu hiyo irudishwe Jeshini na Mhe. Abdalla Mwinyi Khamis alipwe fidia, ambapo wizara yako ilitekeleza agizo hilo. Jambo la kushangaza, kuna taarifa kwamba baada ya kuundwa uongozi wa serikali ya awamu ya saba, wizara hiyo ilimuandikia Mkuu wa Kambi ya Jeshi, Welezo kwamba nyumba iliyokuwa ya Abdalla Mwinyi Khamis imeuzwa kwa Mamlaka ya Maji, yaani (ZAWA).

(a) Je, taarifa ya nyumba hiyo kuuziwa ZAWA ni sahihi baada ya kulipiwa fidia hapo kabla.
(b) Je, ni nani aliyeuza nyumba hiyo kwa ZAWA wakati tayari Mhe. Abdalla Mwinyi Khamis alishalipwa fidia na nyumba hiyo kukabidhiwa Jeshi Kambi ya Welezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 71 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo machache kwa suala hili. Mhe. Spika, wizara yangu inakiri kuwa ni kweli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ilipima viwanja kwa ajili ya makaazi ya wananchi katika eneo la Welezo, baada ya kuanza kujengwa kwa viwanja hivyo, Jeshi la Wananchi wa Tanzania waliifuata serikali na kuomba kuondolewa eneo hilo kuwa ni eneo la makaazi ya wananchi.

Mhe. Spika, serikali katika kulitekeleza hilo, tayari ilimkuta Mhe. Abdalla Mwinyi Khamis ambaye yeye ni miongoni mwa wananchi waliopewa viwanja katika eneo hilo,

akiwa ameshajenga na kutakiwa kulipwa fidia. Mhe. Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania wakawa tayari kufanya hivyo ili wapate kulimiliki na kuitumia nyumba hiyo.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilitafakari kwa kina na kuamua kuwa kupitia Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, italipa fidia hiyo na kulichukua jengo hilo kwa ajili ya kutumika na moja ya taasisi zake.

Mhe. Spika, baada ya hapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ilitekeleza uamuzi wake huo na kukabidhi nyumba hiyo kwa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa wakati ule, na wizara hiyo kuamua kuikabidhi nyumba hiyo kwa Mamlaka ya Maji Zanzibar, kwani ni taasisi yake ambayo ina vyanzo vya maji karibu na maeneo hayo pamoja na miundombinu mingine ya maji kama vile matangi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama hivi ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, kutokana na maelezo ya awali, ZAWA haijauziwa nyumba hiyo, bali ZAWA imekabidhiwa nyumba hiyo na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi.
(b) Mhe. Spika, kwa mujibu wa jibu mama (a) hakuna aliyeuza nyumba hiyo kwa ZAWA.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri, kwa sauti yake ndogo leo kidogo ambayo hatuifahamu vyema. Baada ya hapo niulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba eneo lile wizara yake iligawa viwanja na miongoni mwa wananchi waliopewa ni Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Mhe. Abdalla Mwinyi Khamis.

Mhe. Spika, kwa kuwa Jeshi walijenga hoja na kusema kwamba eneo lile ni eneo la Jeshi, halipaswi kukaa raia na hatimaye wakaamua nyumba hiyo Jeshi kuichukua kwa taarifa za mwanzo, lakini kumbe nyumba hiyo ilichukuliwa na wizara yenyewe.

(a) Je, Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri haoni kwamba hiyo ilikuwa ni mbinu maalum ili wananchi wengine wanyonge ambao walipewa viwanja sawa sawa na Mkuu wa Mkoa, kunyang'anywa ardhi ile.

(b) Mhe. Spika, kama hoja ni kuwa lile ni eneo la Jeshi, kwa nini leo wizara ichukuwe nyumba ile wamepe Mamlaka ya Maji badala ya kupewa Jeshi wenyewe, hiyo si mbinu maalum kwa ajili ya kuwanyonga wanyonge.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza nataka nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba hakuna mbinu yoyote ya kunyang'anywa wananchi maeneo yale.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza mwanzo kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imeinunua nyumba ile na kuikabidhi Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na ni kwa sababu maalum, kwamba pale ni sehemu ambayo ina vianzio vya maji ambavyo vinahusiana na taasisi zake.

Utaratibu

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, utaratibu ni kwamba naomba Mhe. Naibu Waziri anijibu nifahamu, kwa sababu hoja yangu ni kwamba Jeshi walichukua nyumba ile kwa hoja ya kwamba ni eneo la Jeshi. Sasa ni tofauti ipi baina ya Mamlaka ya Maji na wananchi, hiyo sheria ya sasa hivi ni kwa mamlaka. Naomba nijuwe hilo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa ruhusa ya kuongezea katika majibu mazuri aliyotoa Mhe. Naibu Waziri kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Naibu Waziri kwamba serikali haikuwa na ujanja wa kuwanyang'anya wananchi maeneo yale, bali Jeshi walikuwa wanazungumzia maeneo yale yapo karibu na vituo vyao, na kwa hivyo wakataka wananchi waliopewa maeneo yale wahamishwe na nyumba ile hususan ya Mhe. Abdalla Mwinyi Khamis ichukuliwe. Nyumba ikalipiwa fidia na serikali ndio wakapewa mamlaka kwa maana ya afisi ya serikali kutumia kama ni afisi yao. Kwa bahati mbaya Jeshi wameendelea kujenga hoja na nyumba ile sasa wameichukua na hivi sasa inatumiwa na Jeshi, haitumiwi na ZAWA. ZAWA imelalamika lakini bado hakuna kilichofanywa. Kwa hivyo, nyumba ile sasa inamilikiwa na Jeshi.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa eneo lile tayari limeshapimwa na serikali, na wananchi wamekabidhiwa eneo lile au viwanja katika eneo lile na baadhi yao wengine walishaanza kuvishughulikia viwanja vile.

Je, serikali ina mpango gani wa kuwafidia viwanja vyengine wale wananchi ambao tayari wameshapewa viwanja katika eneo lile kwa ajili ya ujenzi, ili wananchi wale wapate nafasi sasa na wao kujenga makaazi mengine.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nakushukuru. Mhe. Spika, serikali imeshawafidia baadhi ya wananchi waliohamishwa katika eneo lile, wengine bado wako katika mpango wa kufidiwa. Kama bado watakuwa wamo katika lile eneo ambalo Jeshi wamesema ni eneo ambalo halifai kukaa raia. Kwa hivyo, hatua za kufidia zimechukuliwa, baadhi ya wananchi wamepewa viwanja Tunguu na bado viwanja vipo kama kuna wananchi watapenda kuondoka pale kwa usalama wao, wakahamie pahala pengine, basi serikali ina uwezo wa kufanya hivyo.

Nam. 79

Ada ya Upasuaji kwa Wazazi

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu wananchi wengi hasa kinamama wamekuwa wanalalamika kwa utozaji wa Tshs. 40,000/= kwa huduma za mama mzazi anayefanyiwa upasuaji kutokana na hali zao ngumu za maisha.

(a) Je, Mhe. Waziri unaweza kueleza Baraza lako tukufu mchanganuo wa gharama hizo kwa mwaka katika Bajeti ya Wizara na kwamba huoni kwamba sasani wakati umefika kwa gharama hizo kupunguzwa na kubakia angalau Tshs. 20,000/=.

(b) Serikali ina tamko gani juu ya fedha wanazotoleshwa wananchi kwenye vituo vya Afya kabla ya kupewa huduma.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 79 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, gharama kwa mwaka inategemea idadi ya wazazi waliofanyiwa upasuaji. Wizara inawajibika kulipigia gharama kwa idadi hiyo hiyo ya wazazi waliofanyiwa upasuaji. Kiwango cha Tshs. 40,000/= ni sawa au chini ya asilimia 27 ya gharama za upasuaji, na serikali hulipia ile sehemu ya huduma ambayo iliyobakia.

(b) Mhe. Spika, serikali inatambua na kuthamini ushirikishwaji wa wananchi katika kuimarisha huduma za afya, katika maeneo yao kupitia Kamati za Afya za Shehia na Majimbo. Michango hiyo inayotolewa na wananchi, husaidia kuwalipa walinzi kwa usalama wa mali za kituo, kununua baadhi ya vifaa vya uchunguzi wa maradhi na usafi pale vinapokosekana ili huduma ziendelee bila usumbufu. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Mhe. Waziri, mimi ni mmoja kati ya wadau wako katika Wizara ya Afya mkubwa. Hiki kilio cha wazee wetu kimekuwa ni cha muda mrefu na kimekuwa ni usumbufu kulipa Shs. 40,000/= na hufika kuweka vitu vyao dhamana katika ma- *pharmacy* ili kupata huduma au vifaa vya kujifungulia.

Je, Mhe. Waziri, una mpango gani wa kuliondosha suala hili na ikiwa hii ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Vile vile kama livyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba wananchi wetu ni wasikivu.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, umesikiliza kwa makini sana hilo swali.

Mhe. Waziri wa Afya: Ehee. Kwa sababu *speed* kubwa sana, papapa. Lakini nadhani nimemuelewa. Anasema suala hili ni la muda mrefu na kwamba wazazi ni wanyonge na tuna mpango gani. Nadhani hivyo ndivyo nilivyomsikia.

Mhe. Spika, naomba nirudie kwamba suala hili, lilijitokeza sana wakati wa bajeti na swahib yangu Mhe. Salmin Awadh alilijadili kwa upana sana. Katika majibu yangu kwa wakati ule nilisema kwamba nitarudi kwenu kuja na jibu. Lakini sio suala linalotaka jibu la ghafla, kwa sababu linahusu kuitizama shughuli yote nzima kwa pamoja. Unapoondoa Shs. 40,000/- za kinamama ni lazima uwe tayari umeshazipata pahala pengine kuweza kufidia. Sasa ili uzifidie inabidi aidha uongeze gharama katika huduma nyengine zifidie pale au uchukuwe wastani wa gharama zote, halafu uzifanye kwa wastani, iwe mtu yeyote anayeingia hospitali pale analipa kima hicho ili kusaidia wale wanyonge.

Mhe. Spika, naendele kulifanyia kazi hili na kwa sababu mimi mwenyewe kidogo ni mtu ambaye najua nambari, basi huwa nachukua hima mimi mwenyewe, hukaa na wale madaktari na wafanyakazi wa hospitali mpaka wananishangaa kwamba huyu waziri gani anakuja mpaka kutuuliza ili ajuwe undani huo. Nimeshamaliza idara moja, naendelea na nyengine.

Mhe. Spika, vile vile wananchi wakumbuke kwamba Baraza hili limetutaka tuchange milioni 540 kama ni sehemu ya mchango wa wananchi. Sasa utakapokata ghafla ukazifanya 20,000/- na hizi 20,000/- itabidi zitafutwe mahali pengine ili kutimiza hii ahadi ya Baraza. Kwa hivyo, narudia kumwambia Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwamba kazi naendelea kuifanya na hapa nina wastani wa kila sehemu ya hospitali ile ni michango kiasi gani kwa kipindi kilichopita. Nikimtajia hiyo *scissors* tu imekusanya milioni 13, lakini imetumia milioni 14.5 ina-*deficits*. Kwenye idara ya maabara, imekusanya milioni 10 na imetumia milioni 14. kiingilio kinachotoka wizara ya fedha, tulielezwa na Mhe. Waziri hapa kwamba kipindi hiki kuna ufinyu wa mapato.

Kwa hivyo, suala hili ni la kibajeti, halitaki maamuzi ya ghafla, linataka maamuzi ya uangalizi wa zile takwimu na jinsi ya kulitatua. Sera yetu ya *cost sharing* ililikubali kwamba wananchi wachangie. Hiyo nitakuja nayo nikikamilisha hapa kwa maamuzi ya mwisho, ili nipate kibali. Wakati huo nadhani tutakuwa na sura kama hii.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Spika, kwa kuwa michango mingine hospitali hutolewa bila ya kuwa na risiti, kitu ambacho hupelekea kuvuja kwa mapato hayo ambayo ndio tegemeo la wizara na serikali kwa jumla.

(a) Je, Wizara yako kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, mna mpango gani wa kuhakikisha kwamba hospitali zote na vituo vya afya kunakuwa na risiti rasmi za serikali.

(b) Kwa kuwa umezuka mtindo kwa baadhi ya watendaji ambao sio waaminifu, kuitumia fursa hii ya kutozwa michango kwa baadhi ya huduma wao hutoza michango kwa kila aina ya huduma hata ile ya kufunga vidonda. Je, Mhe. Spika, Mhe. Waziri anatoa wito gani kwa wananchi wanaokumbwa na kadhia hiyo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, suala la risiti ni suala ambalo tumekubaliana na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwamba tutumie risiti zile za wizara ambazo sio rahisi kuzichakachua. Shughuli hiyo bado inaendelea na pale Hospitali ya Mnazi Mmoja suala hili limeanza kufanyika kwa baadhi ya idara, lakini tunaendelea. Nahakikisha baada ya mwaka kumalizika tutakuwa tumelimaliza, kwa sababu linahitaji utaratibu.

Mhe. Spika, kwa kuthibitisha hivyo. Hivi karibuni kuna mkusanyaji wetu wa fedha pale Hospitali ya Mnazi Mmoja, alitaka kuchakachua shilingi milioni 6 alizozikusanya, lakini kwa sababu ule mfumo umeanza kukaa, mara moja tukamgundua na tukamshika. Kabla ya kumpeleka kokote tukamwambia ufe upone lakini pesa zetu utupe kwanza. Akazirejesha. Kwa hivyo, inaonekana kwamba ule mfumo unaanza kuchukua sura, kwani hapo zamani ilikuwa kila mtu *Lailah Hailallah Muhammad Rasulullah*.

Mhe. Spika, kuhusu suala la kwamba kila aina ya huduma ule waraka ambao uko kwenye hatua ya mwisho utaeleza ni taratibu gani zinazotakiwa, ni nani anastahiki kusamehewa na ni aina gani ya huduma zinahisi kulipiwa. Mhe. Spika, itabidi hizo ziandikwe kwenye *notice board* kila mwananchi ajue na mimi nitachukua hima kutangaza kwamba unapokwenda kutaka huduma hii usilipe zaidi ya hiki, kwa hiyo mwananchi mwenyewe atakuwa ni mlinzi wa maslahi yake.

Nam. 21

Walimu Wenye Viwango kwa Timu ya Taifa ya Zanzibar

Mhe. Abdi Mosi Kombo - Aliuliza:-

Mchezo wa mpira wa miguu ni miongoni mwa ajira kubwa ulimwenguni. Kwa kuwa Zanzibar kiwango cha uchezaji cha mpira wa miguu kipo chini kutokana na kukosa taaluma bora na walimu wenye viwango vinavyotakiwa.

Je, Mhe. Waziri Wizara yako ina mpango gani wa kutafuta walimu wenye viwango ili kuinua hali ya soka nchini pamoja na kuwapatia kipato wana michezo wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 21 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli nakubaliana na hoja hii kwamba mchezo wa mpira wa miguu ni miongoni mwa ajira kubwa kwa vile tumekuwa tukishuhudia pamoja na kusikia viwango vikubwa vya fedha ambavyo wachezaji wa mpira wa miguu wamekuwa wakilipwa au kununuliwa kutoka timu moja kwenda nyengine.

Mhe. Spika, wizara yangu iliona kuna umuhimu mkubwa wa kupata walimu wenye viwango kwa mashirikiano na nchi mbali mbali kama vile Misri, Cuba na kadhalika. Tayari mazungumzo na makubaliano (*MOU*) yameshafanyika kati ya wizara yangu na Serikali ya Cuba pamoja na Misri ili waweze kutupatia wataalamu wa fani hii ili waendelee na wataalamu wetu waliopo kuinua kiwango cha soka hapa Zanzibar na kuwapa matumaini makubwa vijana wetu. Pamoja na juhudi hizo tayari tunao wataalamu wachache wanaotambulika na *FIFA* na wanaendelea kuwafundisha vijana wetu.

Kwa mfano – Kocha kutoka Misri Abdulsatar Abass (*Karume Boys*) pamoja na wataalamu wazalendo.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri wizara yake ina mpango gani wa kuagiza kocha wa *netball.*

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu mama kwa sababu wataalamu hawa hatuchagui kama kuna kocha wa *netball* na kocha wa *football* wote ni makocha ambao wanaweza kufundisha kwenye michezo mengine.

Mhe. Ali Salim Haji: Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Chama cha Makocha Zanzibar kimeanzisha taaluma pale Skuli ya Haile Salassie kupitia makocha wetu wazalendo akiwemo Kocha Msoma, Jabir na wengineo, ambapo taaluma yao makocha wale inawapa uwezo wa kufundisha soka ndani ya Zanzibar.

Je, Mhe. Naibu Waziri haoni kwamba kuna haja ya kutafuta mashirikiano ya kuwatafuta walimu wa ziada kutoka Tanzania Bara ambao ni Ndugu Charles Boniface Mkwasa na Ndugu Kayuni ambao uwezo wao wa kuja kusomesha hapa utawapa makocha wetu wa Zanzibar kuweza kufundisha soka mpaka katika Afrika.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, mimi nakubaliana na Mhe. Mwakilishi na ninakuamini kwamba wewe ni mwana michezo halisi kwa kweli tutashirikiana na Chama cha Soka Zanzibar ili kuwatafuta makocha hao.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa mpira wa wanawake *netball* hivi sasa umekuwa ni adimu kwa Zanzibar tofauti na enzi za huko nyuma. Je, Mhe. Naibu Waziri ni sababu zipi ambazo zimerejesha mpira huo hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, namwambia Mhe. Mwakilishi kwa kweli mimi mwenyewe binafsi nimeshatembelea timu ambazo ziko Kusini Pemba na Kaskazini Pemba kwa kushirikiana pamoja na Mhe. Waziri wangu tukaweza kuzungumza nao na tukasema kwamba tutaweza kukaa nao pamoja ili kuwatafutia makocha ambao wapo hapa Zanzibar na wakiwa ni wanawake. Kwa hivyo, mimi naomba mashirikiano yako Mhe. Mwakilishi ili tuwe pamoja tuweze kuziendeleza timu hizo kwa upeo zaidi.

Nam. 83

Uingizaji wa Nyama ya Kuku Kutoka Nje ya Nchi

Mhe. Salum Amour Mtondoo - Aliuliza:-

Hivi karibuni imejitokeza tabia ya kuingiza Zanzibar Kuku waliochinjwa kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kuuzwa hapa Zanzibar.

(a) Je, Serikali ilifanya utafiti wowote unabainisha upungufu uliopo wa kuku na haja ya kuingizwa kuku kutoka nje.

(b) Huoni kwamba uingizaji wa kuku hao unahatarisha juhudi za wafugaji wetu na kunufaisha zaidi wafanyabiashara wachache matajiri kuongeza utajiri wao na kuwaacha maskini zaidi wafugaji wetu.

(c) Tahadhari kiasi gani kiafya zinachukuliwa kuona kama kuku hao wanafaa kwa matumizi ya binadamu

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 83 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi haina taarifa ya kwamba hivi karibuni kumejitokeza tabia ya kuingiza Zanzibar kuku waliochinjwa, ila taarifa niliyopewa na inayofahamika ni kwamba nchi yetu Zanzibar ni muagiziaji wa bidhaa mbali mbali za chakula hasa mchele, sukari, unga wa ngano, nyama za vibati na hivi karibuni nyama ya kuku kwenye maboksi. Kwa sababu Wizara ya Mifungo na Uvuvi haina taasisi zenye jukumu la uagizaji bidhaa hizo, hapana shaka zimefanya wajibu wake kabla ya chakula hicho hakijaingizwa nchini.

Nam. 24

Ziara kwa Wafanyakazi

Mhe. Hassan Hamad Omar – Aliuliza:-

Ufanisi wa kazi unaweza kupatikana kwa kiongozi kuweka utaratibu wa kukutana na wafanyakazi wa chini yake ili kujadili kwa pamoja changamoto zinazowakabili katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, utaratibu huu haupo au kama upo haueleweki vizuri.

a) Je, Mhe. Waziri huoni kuwa tatizo hilo linazorotesha maendeleo na ufanisi wa kazi za kila siku.

b) Je, Mhe. Waziri una mpango gani wa kuweza kukutana na wafanyakazi wa wizara yako ili kujadili changamoto zinazowakabili katika kazi zao za kila siku.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 24 lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa ufanisi wa kazi unaongezeka pindipo viongozi wanapokuwa na utaratibu wa kukutana na wafanyakazi wake wa ngazi zote ili kujadiliana nao juu ya changamoto zinazowakabili sehemu zao za kazi na jinsi ya kuweza kuzitatua. Kwa upande wa wizara yetu ni kwamba utaratibu wa viongozi wa wizara kukutana na watendaji wa ngazi za kati na ngazi za chini umekuwepo muda mrefu na unaendelezwa. Tokea kuteuliwa kushika dhamana hii tumefanya vikao mbali mbali katika idara zote za wizara na Walimu Wakuu katika baadhi ya Wilaya. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, wizara yangu ina utaratibu wa kuonana na wafanyakazi wa ngazi za kati na ngazi za chini na kujadiliana nao juu ya matatizo yanayowakabili na utaratibu huu unasaidia katika kuleta maendeleo na ufanisi wa kazi. Viongozi wa wizara mara kwa mara wamekuwa wakikutana na wafanyakazi katika vikao mbali mbali na katika ziara ya ufuatiliaji kazi kwa taasisi zetu katika sehemu mbali mbali za Unguja na Pemba.

b) Mhe. Spika, tokea kuteuliwa kushika dhamana hii viongozi wakuu wa wizara wamekuwa wakifanya ziara katika idara zote za wizara yetu kwa mfano. Tumefanya vikao na kutembelea majengo na wafanyakazi katika idara zote, vile vile tumefanya mikutano na wahadhiri na wafanyakazi wa Chuo Kikuu

cha Taifa cha SUZA. Pia tumefanya vikao na kuzungumza na Walimu Wakuu wa Wilaya za Wete na Micheweni huko Pemba.

Vile vile tumekutana na kubadilishana mawazo na viongozi wa chama cha walimu Zanzibar (ZATU) na Jumuiya ya Umoja wa Skuli Binafsi (ZAPS). Aidha, tumetembelea skuli mbali mbali za Unguja na Pemba na kukutana na walimu na wanafunzi na kuzungumza nao kuhusu maendeleo na matatizo yanayowakabili sehemu zao za kazi, na hatua tunazopanga kuchukua kukabiliana na changamoto hizo. Ziara hizo zinaendelea mara kwa mara.

Mhe. Hasaan Hamad Omar: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Naibu Waziri alipokuwa anajibu alisema kwamba wanatembelea wafanyakazi wao. Je, ni changamoto gani mlizozipata wakati mlipotembelea sehemu ambazo umezitaja.

b) Kuna mafanikio gani mliyoyapata.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, wakati wa ziara zetu ambazo tulikutana na watendaji wetu, kuna changamoto kadhaa ambazo tulikutana nazo moja wapo ikiwa ni vitendea kazi hafifu na visivyotosha katika kufanya kazi zao. Lakini Mhe. Spika, suala lake la (b) kuhusu mafanikio ni kwamba yanapatikana kwa sababu changamoto hizi tunazifanyia kazi hatua kwa hatua.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipatia fursa hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Kwa kuwa wadau wakubwa wa Wizara ya Elimu ni walimu na sio wafanyakazi. Je, haoni kwamba kuna kasoro ya kutokuwatembelea wale walimu akaendelea kutembelea wafanyakazi.

b) Katika ziara ya skuli kwa skuli hapa Unguja kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja yeye na Mhe. Waziri wametembelea skuli ngapi za Unguja na skuli ngapi za Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwenye jibu langu mama nilieleza kwamba ziara hizi tumeonana na watendaji na pia tumeonana na walimu wakuu pamoja na walimu wa kawaida na wanafunzi. Nadhani hakunielewa, lakini kwenye skuli za Unguja kama nilivyosema kuwa ziara hizi bado zinaendelea ni kwamba tumeanzia Pemba na sasa mwelekeo wetu ni kutembelea skuli za Unguja.

Nam. 29

Mafunzo ya Sheria ya Usalama Barabarani kwa Wanafunzi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kuna wakati Jeshi la Polisi lilitangaza kuwa litatoa mafunzo kwa wanafunzi maskulini juu ya mambo yanayohusu usalama kwa lengo la kupunguza ajali barabarani na kuepusha vijana na vitendo vya uvunjaji wa sheria za barabarani bila kukusudia. Hata hivyo kuna taarifa kuwa Jeshi la Polisi tayari limetayarisha walimu kwa ajili ya mafunzo hayo, lakini mafunzo hayo hayakufanyika kwa sababu Jeshi la Polisi kukosa mashirikiano katika Wizara ya Elimu.

(a) Je, Mhe. Waziri unaelewa hali hiyo ya Wizara yako kutotoa mashirikiano kwa Jeshi la Polisi kwa ajili ya mafunzo hayo.

(b) Kwa kutotoa ushirikiano unaohitajika, Wizara ya Elimu haioni kuwa imewakosesha vijana wetu mafunzo muhimu sana kwa ajili ya usalama wao wanapokuwa barabrani.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe, Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 29 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa jeshi la Polisi Tanzania limepenga kutoa mafunzo kwa wanafunzi maskulini juu ya masuala ya Usalama Barabarani kwa lengo la kupunguza ajali za barabarani na kuwaepusha vijana na vitendo vya uvunjaji wa sheria za barabarani bila ya kukusudia. Mafunzo hayo yameandaliwa kwa kupitia kauli mbiu inayojulikana kwa jina la **"USALAMA WETU KWANZA**". Wizara yangu inalipongeza sana Jeshi la Polisi kwa kubuni mafunzo hayo kwani utekelezaji wake utasaidia sana katika kupunguza ajali barabarani miongoni mwa wanafunzi, lakini pia kupunguza utoro wa wanafunzi maskulini.

Wizara yangu imeshirikiana kikamilifu na Jeshi la Polisi katika suala hili na viongozi wa wizara walikutana na viongozi wa Jeshi la Poilisi katika mwezi wa Septemba, 2010 walikutana kwa ajili ya kupanga mikakati ya jinsi ya kutekeleza mafunzo hayo. Hata hivyo, suala hilo halikuweza kutekelezeka katika kipindi hicho kutokana na Polisi kukabiliwa na jukumu kubwa la ulinzi na usalama wakati wa kipindi cha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010. Hivyo, dhana ya kwamba wizara yangu haikutoa mashirikiano kwa Jeshi la Poilisi haikuwa sahihi.

Baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa napenda kutoa majibu yafuatayo:-

a) Wizara yangu inayo mashirikiano mazuri na Jeshi la Polisi na ndio maana skuli zetu nyingi zilizoko karibu na barabara kuu, askari wa usalama

barabarani wamekuwa wakitoa msaaada mkubwa katika kuwaongoza wanafunzi kukatisha barabara hasa nyakati za asubuhi na wakati wanafunzi wanapomaliza masomo yao mchana na jioni. Napenda kutoa pongezi zetu za dhati kwa Jeshi la Polisi kwa jinsi wanavyolitekeleza jukumu hili.

b) Suala la usalama barabarani ni muhimu sana kwa wanafunzi wetu na wizara haijawakosesha wanafunzi kupata mafunzo. Napenda ieleweke mada za usalama barabarani ni sehemu za mada katika mitaala yetu ya elimu ya msingi na hivyo kwetu sisi ni faraja kwa Jeshi la Polisi kuwa tayari kutoa mafunzo kwa walimu wetu juu ya namna ya kuzifundisha mada hizo. Ni hivi karibuni tu tumefanya mkutano wa viongozi wa Jeshi la Polisi na kukubaliana juu ya utaratibu wa kuendesha mafunzo hayo na tunatarajia kuanzia katika skuli za msingi hivi karibuni.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri kabisa naomba kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Naibu Waziri utakubaliana na mimi kwa hayo mafunzo yaliyofanyika mara moja tu katika Skuli ya Vikokotoni na baada ya hapo yakasita na ni sababu zipi zilizosababisha kusita kwa mafunzo haya.

b) Kwa kuwa Jeshi la Polisi bado lina nia ya kuendelea na mafunzo haya katika Skuli za Unguja na Pemba. Je, wizara yako ina mpango gani kuendeleza shughuli hii muhimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba mafunzo haya yamefanyika Skuli ya Vikokotoni tu, na sababu ambayo ilisababisha ipate skuli hiyo tu mafunzo ni zile ambazo nilizieleza katika jibu langu mama wakati ule ilikuwa tunakabiliana na uchaguzi mkuu. Kwa hivyo, Jeshi letu la Polisi lilikuwa na kazi nyingi za kusimamia uchaguzi huo, lakini kama nilivyoeleza ni kwamba tumekutana karibu vikao vinne na Jeshi la Polisi na utaratibu wa kutoa mafunzo tayari umeandaliwa na karibuni mwezi unaokuja tutazindua rasmi mpango huu na tutaanza kuuzindua katika Skuli ya Kiembesamaki.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kitu kizuri na chenye manufaa huwa hakitaki majaribio mengi, kikishagundulikana kitu kizuri basi hutekelezwa. Ni sababu zipi za msingi zinazopelekea hata mara hii baada ya kumalizika huo uchaguzi mkuu baada ya mwaka mzima kumalizika uchaguzi mkuu, ikawa ni skuli moja tu tena ndio iliyochaguliwa Unguja na Pemba. Ni kwamba hakuna polisi wa kutosha wa kutoa mafunzo au wanafunzi wamekwenda likizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nataka nikubaliane na yeye kama suala zuri sio uzuri kulifanyia ajizi, lakini kama nilivyoeleza kwenye jibu langu mama kuwa hatujafanya ajizi baada ya uchaguzi tu tayari tumeshakaa na Jeshi la Polisi karibu vikao 4. Tumekaa nao kikao cha kupanga nao, tumekaa nao na walimu wakuu wa Wilaya zetu hususan Wilaya ya Mjini Magharibi kupanga nao, tumekaa na

Kamishna kumkumbusha juu ya mpango huu. Pia hata juzi tumekaa nao kupanga utaratibu wa ratiba namna ambavyo utakuwa.

Mhe. Spika, nataka nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kama kwanza kulikuwa na tatizo la hawa walimu wa kutoa mafunzo walikuwa ni wachache na ndio maana mpango ule tukauelekeza katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Lakini juzi Kamishna ametueleza kama tayari sasa wana walimu wa kutosha kwa hiyo sasa tutaweza kutoa mafunzo haya kwa Zanzibar nzima. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mpango huu utaaanza mara moja kama hali itakaporuhusu.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali ya 2011

(*Majadiliano yanaendelea)*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwanza naomba kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii na mimi kujaribu kutoa maelezo kuhusiana na hoja mbali mbali ambazo Waheshimiwa Wajumbe walichangia kuhusiana na hoja hii ya Mswada wa Marekebisho ya Sheria mbali mbali.

Mhe. Spika, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa michango mbali mbali ambayo wameitoa. Michango iliyotolewa imetolewa na wajumbe kumi, kwa kweli katika michango hii kumekuwa na maoni ambayo ni mazuri, kumekuwa na mawaidha yaliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe ambayo yatatusaidia katika kuimarisha sio tu hii sheria, lakini usimamizi wa sheria wenyewe. Lakini pia kumekuwa na hekima na busara mbali mbali zilizotolewa Waheshimiwa Wajumbe pia wametoa indhari juu ya athari ya dawa za kulevya na fedha haramu. Mhe. Spika, pia kumetolewa rai za marekebisho na kuimarisha usimamizi wa sheria. Hata hivyo, kumekuwa na baadhi ya maswali ambayo yanahitaji ufafanuzi.

Mhe. Spika, kwanza nitangulie kuwataja Waheshimiwa Wajumbe ambao walichangia katika hoja hii nao ni:-

a. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala
b. Mhe. Ali Abdalla Ali.
c. Mhe. Abdalla Mohammed Juma
d. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
e. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
f. Mhe. Rashid Seif Suleiman
g. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
h. Mhe. Asha Bakari Makame
i. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji
j. Mhe. Hamza Hassan Juma
j

MMMMMMMMMMMMMMMMMMMMMMMM

JOKHA 4

Mhe. Mwanasheria Mkuu: (anaendelea) Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Salmin Awadh Salmin. Kwanza Mhe. Spika, naomba nijielekeze katika zile hoja za kijumla, kuna hoja sijui niseme ni mbili kubwa ambazo waheshimiwa takriban wote waliochangia walizigusia.

Hoja ya kwanza ni tume kuwa na wajumbe wengi mawaziri. Hoja hii ilitolewa na Mhe. Abdalla Mohammed, Mhe. Rashid Seif na Mhe. Makame Mshimba pia. Nashukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais alijaribu kufafanua suala hili na kueleze umuhimu wa kila mjumbe ambaye yumo katika tume ile. Lakini mimi naomba niongezee machache kuhusiana na suala hili.

Hoja ya kwanza ni kwamba kwa kipindi kirefu usimamizi wa suala la dawa za kulevya tulikuwa tunadhani ni tatizo la polisi, yaani kwamba hii ni kazi ya polisi kusimamia na kwamba wao ndio kazi yao. Lakini dunia kwa sababu hili ni tatizo la dunia Mhe. Spika, kila wakati imekuwa ikitafakari mbinu bora ya kupambana na suala hili na serikali yetu imekuwa ikifuatilia kwa karibu juhudi za ulimwengu katika kupambana na suala hili na miongoni mwa mambo yaliyopendekezwa katika mikutano, katika mafunzo mbali mbali ya kitaaluma kuhusiana na masuala haya ni kwamba serikali yenyewe lazima iwe karibu sana katika usimamizi wa suala hili.

Kwa ufupi hoja iliyotolewa ni kwamba hili si suala tu la *Law Enforcement*, lakini ni suala la kisera na inatakiwa serikali ili juhudi hizi ziweze kufanikiwa lazima iwepo karibu sana katika kusimamia suala hili la kudhibiti dawa za kulevya. Na kwa maana hiyo, ndio maana kwamba miongoni mwa mapendekezo yaliyotolewa na taasisi na jumuiya mbali mbali ikiwemo Tume ya Umoja wa Mataifa ya Kupambana na Madawa ya Kulevya basi ni kubadili muundo wa usimamizi kwa kuwa na chombo cha kisera ambacho kitasimamia na kitatoa maamuzi ya haraka kwa mambo mbali mbali, halafu kuwe na chombo cha kitaalamu halafu daraja ya tatu ndio kuweko na hizi *operation* (*Law Enforcement Agencies*).

Kutokana na ushauri huo ndio maana Mhe. Spika, utakuta kwamba takriban nchi zote zina mfumo unaofanana na huu wa kwetu tulionao. Ukiangalia Zambia wana kamisheni kama hii ambayo ni ya mawaziri, Tanzania Bara na nchi nyengine mbalimbali kwa sababu hayo ni mapendekezo ya namna bora ya kusimamia. Kwa hivyo, ile tume ya mawaziri na kama ilivyoelezwa jana kwamba suala hili ni mtambuka kila mtu amewekwa pale kwa ajili ya kusimamia na kutoa maamuzi yanapohitajika. Hata ukiangalia kifungu cha 7 cha sheria hii kimetoa kazi ya ile kamisheni yenyewe kwamba ni kusimamia kwa karibu masuala zaidi ya kisera. Lakini baadae ndio kuna chombo cha kitaalamu ambacho nacho kinachukua wataalamu kutoka sehemu mbali mbali na baadae kuna hivi vyombo vya usimamizi wa sheria.

Kwa hivyo, huu si utaratibu wa kwetu tu, lakini ni moja katika mbinu ambayo Jumuiya ya Kimataifa imeona kwamba kuna haja ya kuifuata kama ni njia ya kuimarisha usimamizi wa sheria. Na katika hili nadhani limesaidia kuifanya serikali kuwa karibu zaidi na usimamizi wa suala hili na tumeona kwamba hata wananchi wamehamasishwa

zaidi, lakini bado nakiri kuna haja ya kuimarisha zaidi usimamizi wa suala hili. Kwa hivyo, naomba lisitupe shida hasa nimuombe Mhe. Rashid Seif kwamba ingawa inaonekana

Mhe. Spika: Niwaombe Waheshimiwa Wajumbe, wanaotoka nje Mhe. Mwanasheria Mkuu anafanya majumuishao si muda mkubwa, baadae tunalazimika kupitisha vifungu vya mswada huu. Kwa hivyo, wale ambao wanadharura waelewe kwamba muda mchache ujao tunataka kumaliza shughuli hii na niwaombe basi walioko nje waingie ndani. Mheshimiwa Endelea.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Rashid Seif kwamba hivi ni vita na katika vita nchi yoyote inakuwa na kamati au tume ya mawaziri ambayo inasimamia vita vile. Kwa hivyo hii nayo ni *war cabinet* ulivyosema ina usahihi kwamba bado labda Mwenyekiti na Makamo wa Pili tu wa Rais, lakini ndio nasema ndio hali halisi na ndio inavyotakiwa kuifanya serikali iwepo karibu zaidi na vita hivi vigumu na vikubwa.

Mhe. Spika, naomba niwakumbushe kwamba kwa kweli vita hivi kwanza sio vya leo, kwa sababu tunaweza tukavunjika moyo, tunaweza tukaona labda hatufanyi jambo lolote, lakini hivi si vita vya leo ni vita ambavyo zimeanza zamani pengine huku kwetu zamani ilikuwa ni ndondondo sasa imekuwa chururu ndio tunaona kweli tatizo limekuwa kubwa. Lakini ukitizama historia ya dunia katika kupambana na suala hili imeanza mbali sana, historia ya nchi nyengine imewatanabahisha kwamba kwa kweli hili tatizo ni kubwa na limeanza mbali.

Kwa mfano Wamarekani, juhudi zao za mwanzo walizofanya ilikuwa ni kuunda tume kuisaidia China kupambana na suala hili, kwa sababu katika watu ambao walizidiwa mwanzo duniani na tatizo hili walikuwa ni Wachina. Kwa hivyo, Rais wa Marekani, Theodore Roosevelt mwaka 1909 akaunda kamisheni ikiitwa *Shangai Commission* kuisaidia China kupambana na tatizo hili. Lakini baada ya ripoti ya ile tume aliyounda ikamwambia wewe unasaidia China lakini huku kwako na wewe kumeharibika kweli kweli na ndio maana Wamarekani wakatunga sheria yao ya mwanzo ya *Opium Smoking Exclusion Art* ya mwaka 1909. Dunia nzima ilianza kuchukua juhudi za kupambana na tatizo hili wakati ule Kiswahili tulikuwa tukiita Kasumba, lakini pengine wakati ule waliokuwa mjini walikuwa kidogo, lakini wanajua kama ni tatizo na ndio maana hata hapa Zanzibar sheria ya mwanzo ya kupambana na madawa ya kulevya ilitungwa mwaka 1915, sheria Nam. 5 ya mwaka 1915, hatukupishana sana na Wamarekani ni kwa miaka sita tu.

Lakini hata katika ngazi ya kimataifa utakuta kwamba Umoja wa Mataifa wenyewe uliunda Tume ya Ushauri mwaka 1920 na baadae ikaunda tume maalum *United Nation Commission for Drugs* mwaka 1946. sasa utakuta kwamba hizi juhudi kwa kweli na hili tatizo limeanza mbali sana, maana mpaka sheria imetungwa hapa kwetu mwaka 1915 ni kuonesha kwamba tumekuwa na tatizo hili kwa muda mrefu na dunia yenyewe imekuwa na tatizo hili kwa mura mrefu na juhudi kama vile tunavyoona kwamba hawa

wanaofanya biashara hii nao wanabadilisha mbinu na dunia nayo imekuwa ikibadilisha mbinu na serikali nazo zinabadilisha.

Lakini hoja nyengine ambayo imezungumzwa ni kuhusiana na udhaifu katika usimamizi wa sheria na hasa kesi zetu. Hoja hii ilizungumzwa na Mhe. Ismail Jussa, Mhe. Rashid Seif, Mhe. Makame Mshimba, Mhe. Asha Bakari na Mhe. Hamza Hassan Juma vile vile.

Kwanza nikiri kwamba kuna udhaifu katika usimamizi wa sheria hii, udhaifu huu hautokani na vile tunavyoona kwamba tatizo kubwa labda ni rushwa peke yake, lakini kuna sababu mbali mbali. Miongoni mwa sababu hizo kwanza ni udhaifu katika utendaji wetu. Hivi vita vinahitaji watu ambao kweli wamefunzwa na wanafanya hii kazi kuwa ni *specialization* yao, inahitaji watu ambao wana nyezo, kwa kweli wenzetu wanatumia nyenzo mbali mbali lakini moja katika nyezo kubwa inayotumika sio helkopta peke yake lakini na utafiti. Utafiti ni nyezo kubwa sana kwa sababu utafiti haya ni maradhi ndio utakapoweza kugundua hili tatizo hasa mzizi wake uko wapi, shina lake liko wapi, majani yake yako wapi, kigogo chake kiko wapi na panapoumwa zaidi ni wapi.

Kwa kweli Waheshimiwa kama tutaangalia dunia inavyopambana na suala hili tutaona kwamba wenzetu katika jambo kubwa wanalofanya ni utafiti. Kwa mfano Wamarekani wenyewe, walipotaka kuzidisha mbinu za kupambana na suala hili wewe fikiria tokea mwaka 1934 aliyekuwa Meya wa New York Lagwadia aliunda tume ya kufanya utafiti wa kina kuhusiana na tatizo hili. Wakaja na ripoti na ripoti ile wakaifanyia kazi kuandaa mikakati ya kupambana na tatizo hili.

Ukitizama kuna chombo kimoja kinaitwa *Enter American Antinarcotic Commission*. Hii wamefanya utafiti mpaka takriban kila mwaka juu ya matumizi ya dawa hizi tatizo liko wapi, usafirishaji uko vipi, *enforcement* ikoje, takriban kila mwaka wanafanya utafiti na wanatoa taarifa na kupendekeza mikakati ya kupambana na jambo hili, hii ni tume ambayo iko tokea mwaka 1946 inafanya kazi hizi. Lakini moja katika kazi yake kubwa inayofanya ni utafiti.

Sasa tukubali kwamba katika eneo hilo bado sisi tunaangalia zaidi tulipoanguka lakini tulipojikwaa ndio tuna tatizo la kujua tumejikwaa pahali gani na tutajua tumejikwaa wapi kama tutakuwa tuna utafiti. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nikubaliane tuna tatizo au udhaifu katika usimamizi wa sheria hizi lakini mambo au sababu ni mbali mbali. Mimi naamini kwamba hii tume mpya nguvu mpya iliyopata, mtazamo mpya iliyopata, muamko uliopo naamini itaweza kuandaa mikakati bora zaidi ya kusimamia suala hili na hata huu muundo kwamba sasa imewekewa *technical committee* ya kuchukua wataalamu kutoka sehemu mbali mbali naamini itasaidia katika kuandaa mikakati iliyokuwa bora zaidi.

Pia naomba waheshimiwa tukubali kwamba na sisi mila na desturi zetu alizungumza hapa Mhe. Asha Bakari kwamba moja katika tatizo letu ni muhali. Muhali ni mkubwa sana na muhali hauko serikalini tu, mimi siamini kwamba tunasema hapa kuna watu mapapa wanajulikana hawatajwi. Inawezekana wako wadogo ambao wanaogopa papa, lakini siamini kama Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais ataogopa papa au Mhe. Waziri wake

Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej ambao sasa wamekabidhiwa tume hii. Kwa hivyo, kama huko nyuma kulikuwa na watu wakiogopa nadhani sasa hivi ni wakati wa kupata nguvu ya kuwa basi kama wanawajua kweli wawataje, lakini mimi nasema tatizo ni zaidi ya hilo.

Mhe. Spika, mimi binafsi nimefanya kazi na vyombo vya usimamizi wa sheria kwa zaidi ya miaka 18 kwa karibu zaidi, tokea nikiwa Naibu Mwanasheria Mkuu miaka tisa, kazi yangu kubwa ilikuwa kushirikiana na polisi, nimekuwa Mkurugenzi wa Mashtaka miaka tisa kazi yangu kubwa ni kushirikiana na polisi katika suala hili. Kwa hivyo, ni machache wanayoweza kunidanganya lakini mimi najua ni kwamba tatizo ni zaidi ya hilo ambalo tunalieleza. Tuna kazi ya kufanya na ninaamini serikali itachukua hatua ya kulifanyia kazi eneo hili na nimeona kwamba kuna dhamira mpya, nguvu mpya, ari mpya katika kulisimamia suala hili.

Mimi naomba tuipitishe hii sheria ili tuwape nguvu zaidi wasimamizi wa sheria hii ili waweze kutekeleza na kuyafanikisha yale ambayo pengine huko nyuma yalishindikana. Labda nikiacha hoja hizo za jumla kwa ufupi nieleze zile hoja mahususi za wajumbe.

Kwanza Mhe. Abdalla Mohammed aliuliza suala la kufungwa jengo kwamba inawezekana kukawa na hatari kuwa mtu jengo amekodi na likafungwa yeye hana makosa akaathirika. Lakini ukisoma vizuri sheria ilivyokusudiwa ni kwamba litakalofungwa si jengo kwa sababu ya mmiliki. Kwa mfano, kama mmiliki wa jengo hili amefanya kosa halitofungwa jengo zima itafungwa ile sehemu ambayo amekuwa akiitumia yeye kwa kufanya biashara ile. Kwa hivyo, hiyo hatari au huo wasiwasi kwa kweli haupo kama tutaiangalia vizuri sheria inavyoeleza.

Halafu alizungumzia pengine kuna contradiction baina ya kifungu cha 15(c) na cha 16. Lakini Mhe. Mjumbe ukiangalia vizuri vifungu hivi vinazungumzia vitu viwili tofauti ingawa vimefanana, kwa sababu kimoja kinazungumzia mtu atakayepatikana akiwa na hizi dawa zilizokatazwa na chengine kinazungumzia mtu ambaye amepatikana akiwa ametumia, yaani yule mteja anayechuruza udenda. Huko nyuma utakumbuka kabla ya mwaka 2009 hatukuwa na kifungu cha namna hii. Kwa hivyo, vinazungumzia vitu viwili tofauti ingawa ukiviangalia unaona kama ni vitu ambavyo vimefanana.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis nashukuru kwa busara zako na ulitoa ufafanuzi wa vifungu mbali mbali, lakini nadhani mengi ya marekebisho ambayo uliyataja tayari yalishazungumzwa katika taarifa ya kamati ukiangalia yote yale yameshafanyiwa kazi.

Hoja nyengine zimetolewa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu ambaye ametoa maoni na mawazo ya kitaalamu, namshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais alizijibu au alizitolea ufafanuzi nyingi ya hoja hizo. Lakini niungane naye kwamba kweli tumekuwa na tatizo hili la tabia ya Bunge kutunga baadhi ya sheria na kuzifanya zinatumika Zanzibar kwa mambo ambayo baadhi yake wala sio mambo ya Muungano. Mfano mzuri ni sheria ya madawa ya kulevya, wenzetu walitunga sheria ya madawa ya kulevya nadhani mwaka 1994 wakasema inatumika mpaka Zanzibar na kisingizio chao kikubwa ni kwa sababu mambo yale yanaongozwa na mikataba ya

kimataifa, lakini Zanzibar ikasema hilo si jambo la Muungano na ikatunga sheria yake ya kusimamia dawa za kulevya.

Mfano mwengine ni sheria hii ya fedha haamu pamoja na kuelezana, kukubaliana, kufahamishana mpaka tukakubaliana lakini bado walifanya hivyo hivyo, lakini nashukuru serikali ikasema kwamba hili si jambo la Muungano na sheria yenu haiwezi kutumika huku na ikatunga sheria yak wake. Nashukuru Baraza hili liliipitisha sheria hiyo na sasa tuna sheria ya Zanzibar kuhusiana na masuala hayo.

Hoja nyengine aliyoizungumza Mhe. Jussa ni suala la usafishaji wa fedha nyingi nje ya Zanzibar na aliuliza kwamba hakuna sheria au sheria hii inazungumziaje suala hili?

Mhe. Spika, ukiangalia hii sheria imelieleza wazi, kwanza chini ya kifungu cha pili cha sheria hii ya usafirishaji wa fedha haramu. Maafisa wa *Custom* ni moja katika watu wanaotakiwa kutoa taarifa wanapoona vitendo ambavyo vinaashiria usafishaji wa fedha haramu. Moja katika mambo hayo ni usafirishaji wa fedha nyingi *cash* nje ya nchi.

Lakini kifungu cha 8(2) cha sheria hii kimeweka bayana kwamba Afisa wa Kastamu anaweza kuzizuia fedha anazoona kwamba ni nyingi zimesafirishwa juu ya kile kiwango ambacho kinakubalika mtu kusafirisha fedha. Kifungu cha 18(1) kimesema kwamba mamlaka husika ambayo kwa hapa kwetu ni Benki Kuu ya Tanzania inaweza kuweka kiwango kwamba mtu anaruhusiwa kusafirisha *cash* mpaka kiasi fulani. Kifungu hicho hicho kimeelezwa kwamba, Afisa wa Kastamu anaweza akazizuia fedha zile ambazo zinasafirishwa akiwa ataziona bandarini, *air port* au popote zisitoke nje ya Tanzania kama zitakuwa ni zaidi ya kile kiwango ambacho kimeruhusiwa.

Sasa tatizo ambalo tulano sasa hivi ni kwamba Benki Kuu yenyewe haijaweka kima cha juu ambacho kinaruhusiwa kusafirishwa. Kulikuwa na mapendekezo ya dola elfu kumi lakini majadiliano yamekwenda na wadau mbali mbali mpaka sasa bado hakujawa na uamuzi wa mwisho kuhusiana na kima kipi kinaruhusiwa kwamba ndio cha mwisho kusafirishwa nje ya nchi. Kwa hivyo, hilo tutaendelea kuwasiliana na Benki Kuu ili liweze kufanyiwa kazi na litolewe uamuzi na tuweze kuisimamia hii sheria kwa sababu iko wazi kwenye suala hili.

Mhe. Rashid Seif nashukuru kwanza kwa ushauri wake kuhusu utaratubu wa kuingiza marekebisho katika mswada. Mimi nikiri hata wakati mwengine nilipokuwa najaribu kuyaingiza haya marekebisho kwenye mswada ilikuwa ni kazi kidogo, hivyo naweza kuelewa kwamba ni tatizo kuendelea na utaratibu huu ambao tunao. Lakini ndio utaratibu ambao tumekuwa tukiufuata. Naahidi kwamba tutashirikiana na wenzangu kamati ili tatizo hili tuweze kulirekebisha na mimi naamini kwamba tutapokuwa na utaratibu ule wa kusomwa mara mbili utatusaidia kuja na mfumo mzuri zaidi wa kufanya marekebisho.

Lakini pia nasema kwamba, marekebisho haya tusione labda miswada inakuja vipande vipande hii ni dalili kwamba kamati zinafanya kazi. Hilo mimi nashukuru kwa kweli kwa sababu linatupa changamoto ya sisi tuweze kufanya kazi vuziri zaidi.

Nikiri tatizo ambalo nimelikuta kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ni kwamba tuna upungufu mkubwa wa *staff* wa kushughulikia uandishi wa miswada. Kwa sababu naweza kusema sasa hivi nina *only one qualify person* wa kufanya kazi hizi, huyo aandike *regulation*, aandike miswada, afuatilie *Press*, sasa moja katika kazi ambayo tunayo ni kwanza kuongeza watu lakini na kuwapatia mafunzo na hilo nimeanza kulifanyia kazi naamini huko mbele tunakokwenda hali itakuwa nzuri zaidi.

Suala la askari kutishwa akitaka kukamata papa nadhani Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza amelifafanua zaidi, yeye ni mtaalamu zaidi wa masuala haya nadhani na mimi nijaribu kulieleza. Kuhusu kifungu kinachotoa uwezo wa kufuatilia benki ambazo ni matawi hapa Zanzibar, ni kweli kwamba nyingi ya benki ambazo zinafanya kazi hapa ni matawi ya mabenki ambayo ama yako Tanzania Bara au nje ya nchi.

Sheria yetu iko wazi imetoa tafsiri, ukiangalia kifungu cha pili cha sheria yetu hii ya Usafirishaji wa fedha haramu imetoa tafsiri nini benki, au nini *financial institution*. Kwa hivyo, hilo hakuna tatizo katika ufuatiliaji, ikiwa kutakuwa na tatizo basi hizi benki hata ukija ukifungua *cash box* ikiwa ndio biashara yako basi na wewe ni *financial institution* na unawajibika kufuatiliwa kuhakikisha kwamba una *currier* hao wanaosafirisha pesa, hawa *cash biller* wengine *Bureau de Change* wote. Hizi zote ni taasisi za kifedha kwa mujibu wa sheria hii na wanawajibika kufuata sheria hii na wanapokuwa hawakufuata masharti basi wanapaswa taasisi zinazohusika au vyombo vinavyohusika kuwachukulia hatua ipasavyo. Kwa hivyo, kwamba ni *branch* hilo si tatizo hata kidogo katika usimamizi wa sheria hii.

Lakini la mwisho ni suala la sindikizo la fedha haramu kuwa liliiathiri taasisi za kidini katika kupata misaada. Hili ni kweli lakini lilichangiwa na sekta nyingi, moja naamini Mhe. Rashid Seif atakubaliana na mimi mana yeye anawajua zaidi hao watoaji wa pesa taratibu zao haziko makini, wengine inategemea *waster*, kwamba inategemea *influence* yako tu kujuana nao, unaweza kupewa pesa nyingi tu ukenda ukafanyia kazi bila ya kuripoti, bila ya kutoa taarifa na wako wengi waliotumia *waster* huo vibaya kwa kufanya shughuli ambazo si halali.

Tatizo hili linaendelea sasa hivi sio kwenye Dini ya Kiisilamu tu, hata ukitizama dini nyengine za wenzetu, sasa hivi imekuwa kwa kiasi fulani baadhi ya mambo inakuwa kama ni biashara, mtu anatumia mgongo wa dini anapata pesa lakini anafanya shughuli zake. Sasa kwa sababu ya mambo hayo yaliathiri sana basi sasa hivi utakuta nchi nyingi zimewekwa taratibu na hizi taasisi nyingi zimeweka taratibu ambazo ziko bayana kuhusiana na hizi fedha kuwa zinatoka wapi na zinakwenda wapi hata imewasaidia na wao kujua hizi pesa wanazipeleka wapi na zinafanyiwa nini. Sasa hivi ukiletewa pesa wanataka kujua zinafanyiwa kitu gani na wapate taarifa.

Kwa hivyo, mimi nadhani kuimarika kwa utaratibu huu kutasaidia kurejesha tena hili suala la misaada. Wenzetu nchi nyengine wana taratibu nzuri, kuna nchi kukusanya michango ya dini ni sehemu inayoingia katika mfumo wa kodi kama Wajerumani kuna *Church Tax* sio *tax* hasa ni *contribution*, lakini kila mtu mwisho wa mwezi

akishakukatwa mshahara basi akishachukua moja katika *deduction* ni ule mchango wake aliokubali, kama vile anavyolipa kodi kwa taasisi ile inayokusanya kodi wanachukua zile pesa wanaipelekea taasisi inayohusika. Sasa utaratibu *transparent* inajulikana na nchi nyingi zina utaratibu huo.

Malaysia wana utaratibu mzuri sana wa kukusanya michango ya namna hii. Mimi nadhani ni suala la kuwa na utaratibu na sasa hivi najua Kamisheni ya Wakfu wanaandaa utaratibu hata kwa upande wa zaka ili kuwa na utaratibu ambao ni mzuri zaidi.

Mhe. Makame Mshimba nadhani hoja ile ya mawaziri, nimeshaijibu kwa jumla na pia suala la Mkemia kuongezewa mshahara nadhani kama ataweza kukunong'oneza kwa Oktoba hii, naamini kwamba mambo yake yatakuwa mazuri zaidi kuliko huko tulikotoka, kwa sababu amewekwa katika *category* maalum. Sio zamani alikuwa hajulikani ni mtaalamu au vipi, lakini sasa hivi amewekwa kwamba huyu ni wa ngazi fulani, sawa sawa kama yeye na Naibu Katibu Mkuu kama sijakosea, lakini amewekwa katika *level* ambayo inafahamika.

Mhe. Asha Bakar Makame, mengi aliyoyatoa ni maoni na alisisitiza kwenye suala la muhali katika usimamizi wa sheria. Nakubaliana naye na nadhani nimejaribu kulieleza. Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej nakushukuru kwa ufafanuzi uliotoa mzuri. Mhe. Hamza Hassan Juma kuhusu suala la udhaifu katika usimamizi wa sheria nadhani nimelieleza, urasimu wa mahakamani *one stop center*. Lakini yote nadhani yamekuja na jambo zuri la kwamba ni vizuri tukawa na semina ya pamoja ya kuzungumza suala hili, hata sio lazima semina, maana ukiita semina inatisha kidogo, lakini tuseme mkutano wa pamoja wa kuzungumza suala hili. Pengine aliyonayo yote wasi wasi wake na mashaka yake ayaeleze. Mimi naona hiki ni kitu kizuri na tutashauriana na wenzangu kwamba ni vizuri tukakiandaa, sio lazima wawakilishi wote, lakini wachache tunaweza tukalifanya jambo hili.

Mhe. Spika, ni kweli msema pweke hakosi. Ukimwita polisi atasema utasema yeye malaika, ukimwita mahakama peke yake atakuambia hivyo hivyo na ukimwita DPP atakuambia hivyo hivyo. Lakini tukiwa pamoja tukayaeleza, kwa sababu yapo mengi. Kuna mengi ambayo pengine sio vizuri kuyasema hapa, ni vizuri niyasema pahala ambapo na mwenyewe mtu atapata kujitetea yapo, hayo ya rushwa yapo, ya kukosa uadilifu yapo na yapo mengi yanayozungumzwa ambayo sio ya kweli. Sasa haya yote ni mambo ambayo yapo. Kwa hvyo, nadhani tukikutana kwa pamoja tukaelezana, kila mmoja wasi wasi wake unaweza ukamtoka. Pia mwenye joto lake akapata kulieleza, kwa sababu nia ni kujenga kitu kimoja kwa manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi ninachosema ni kwamba tusivunjike moyo sana. Kama nilivyoeleza kwenye historia kwamba wenzetu tuangalie kuwa tokea miaka hiyo suala hili watu wanapambana nalo, lakini tuna shughulika na binadamu. Wengi ni waumini wa dini ya Kiislamu basi ukiisoma Qurani nadhani takriban *two third* inamzungumzia ubaya wa binadamu, sijui kama kuna sura ambayo utafungua haizungumzii binadamu. Mwenyezi Mungu anamsema binadamu unaweza ukajiuliza ndio aliyemuumba, maana yake anavyosema wewe nimekufanyia hivi hunishukuru, wewe unatabia tatizo hili, binadamu

nimemfanyia hivi nikampa hiki na hiki lakini ana hili, kufuru zilizofanywa na binadamu kumfanyia Mwenyezi Mungu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, tujuwe kuwa tunashughulika na binadamu. Mhe. Mwenyekiti, ingekuwa tunashughulika na kupanga maboksi kuwa yakawe sawa basi tungesema wewe unatatizo. Lakini ukitaka binadamu akae sawa, maana Mwenyezi Mungu ndivyo alivyomuumba. Wanasema wataalamu, nimemsikia Sheikh Mhe. Rashid Seif pale siku moja akisema binadamu kaumbwa na *nafsi ammaratun bissuui*, yaani nafsi ya kupenda maovu. Sasa huo ndio ubinadamu halisi, akiwa mzuri basi ujuwe huyo ni mtu wa ibada kweli kweli. Sasa ndiye tunayeshughulika naye hapa huyo binadamu. Kwa hivyo, hii vita ya kupambana na jambo ambalo binadamu katokea kulipenda lina pesa na lina starehe basi ni gumu sana kupambana nalo, lakini mimi nasema ni wajibu wetu inapotokea mbinu hii sisi tukaja na mbinu nyengine na ndio maana hii sheria inarekebishwa mara kwa mara.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naomba niungane na lile wazo la Mhe. Hamza kwamba ni vyema labda tukafanya kikao cha pamoja ili kuweza kulijadili jambo hili.

Mwisho nimalizie na Mhe. Salmin Awadh Salmin kuhusu jina la sheria. Ukiangalia hizi sheria zinazungumzia jambo moja, lakini duniani utazikuta kila nchi hizi sheria ina jina la aina yake, lakini sheria inazungumzia mambo yale yale, utakuta nchi nyengine inaitwa hivi na nyengine inaitwa hivi. Kama huko tunakotoka zamani ilikuwa ni *OPM* tu, *OPM abuse*, *OPM smoking* basi. Sasa hivi kumeingia wangine wanaita *abuse control* sijui. Lakini la msingi ni kwamba jina la sheria si jambo la msingi sana katika usimamizi wa sheria, kwa sababu jina la sheria sio *substantive provision* yaani sio kifungu cha kutekelezwa katika sheria, yale masharti yaliomo ndani ya vifungu ndio jambo muhimu. Ndio maana unakuta tulikuwa tunaliita hivi tukaona bora tuweke jina ambalo ni zuri zaidi. Sasa hivi ilivyokaa mimi naona ina-*include* na hayo ambayo yamezungunzwa na sidhani kama tuna haja, kwa sababu haipunguzi chochote katika usimamizi wa hii sheria.

Jengine ambalo Mhe. Salmin Awadh aliliuliza ni chini ya kifungu cha 4 ni kwamba kwa nini tafsiri ya polisi inafutwa. Labda suala hili lilikuwa limempa wasi wasi. Mhe. Spika, ukiangalia tatizo tulilonalo ni kuwa ukiangalia ile tafsiri ya polisi iliomo ndani ya sheria sasa hivi ambayo inatumika kwa mujibu wa kifungu cha 27 na tafsiri ya polisi ilioko katika kifungu cha 27 zinagongana. Moja tafsiri inasema awe polisi ambaye ana cheo kisichopungua *staff sergeant.* Lakini kifungu cha 27 ambacho ndio huyo polisi mwenyewe anakifanyia kazi, kinasema asipunguwe cheo cha *sergeant .Staff sergeant* nadhani maaskari wanajua kwamba ni tofauti na *sergeant*. Mmoja ana zile tepe tatu na jiwe na mwengine ni tepe tatu tu sergeant. Kwa hivyo, ili kuondoa huu mgongano ndio maana hii tafsiri ikaondolewa, kwa sababu ile tafsiri ilioko kwenye kifungu cha 27 inajitosheleza.

Suala jengine Mhe. Salmin Awadh alisema kwamba Zanzibar tuna Naibu Kamishna, lakini kwa kadiri tunavyojua sisi ni kwamba Zanzibar sasa hivi ina kamishna wa uhamiaji, kama hajachaguliwa atakuwa ni kaimu, lakini kwa mfumo wa uhamiaji sasa hivi Zanzibar aliopo ni kamishna wa uhamiaji Zanzibar, kama vile polisi wana kamishna

wa polisi Zanzibar, halafu ndio kuna yule kamishna general wa uhamiaji ambaye yuko makao makuu. Kwa hivyo, hiki cheo kilichoingizwa hapa nadhani kinaendana na mfumo wa sasa hivi wa Idara ya Uhamiaji ambao upo.

Jengine Mhe. Mjumbe aliuliza kwamba kutoka Afisi ya DPP asiwe mwanasheria wa serikali, lakini awe ofisa ndio iingizwe pale. Lakini ukiangalia kinachohitajika kwenye ofisi ya mkurugenzi wa mashtaka, pale kuna maofisa mbali mbali. Kuna ofisa wa utawala, kuna ofisa wa utumishi na kuna maofisa wengine mbali mbali. Lakini inayohitajika kutoka ofisi ya DPP ni utaalamu wa kisheria, na waliopo pale kwa mujibu wa sheria nambari 2 ya mwaka 2010 wale wanasheria wanaitwa wanasheria wa serikali. Kwa hivyo, ndio maana sheria hii ikasema kwamba awe ni mwanasheria wa serikali, kwa sababu unaohitajika ni ule utaalamu wa kisheria sio utaalamu wa kawaida wa ofisi ya DPP.

Mhe. Spika, mimi nakubaliana naye kwamba pengine ni vyema badala ya kutumia neno mtu kwenye hii sheria basi tutumie neno ofisa kama ambavyo Mhe. Salmin Awadh alivyopendekeza inapendeza vizuri zaidi kwa sababu kwanza anayehitajika ni mtu wa ile ofisi moja kwa moja na pia awe katika angalau ngazi inayoweza ikasaidia.

Jambo jengine ambalo Mhe. Salmin Awadh aliuliza ni kwamba kwa nini kifungu cha 10(2) kinafutwa. Mhe. Salmin Awadh ni kwamba ukiangalia kifungu cha 10(2) cha sheria, kinasema kwamba ile ripoti ya ile iliyokuwa sekreterieti basi ni lazima kwanza iidhinishwe na katibu mkuu wa wizara ndio iweze kwenda kamisheni. Sasa kwa utaratibu huu mpya tunasema kwamba ile ni *technical committee*, kwa hivyo hakutokuwa na haja tena ya kwamba iidhinishwe na katibu mkuu, kile kijifungu kinaeleza hivyo tu, hakielezi kitu chengine na ndio maana kimefutwa kwa sababu sasa hivi kitakuwa hakina haja tena.

Jengine ambalo Mhe. Salmin Awadh amelizungumza ni kwamba wakati ilipopitishwa sheria hii ya fedha haramu kulikuwa na hoja hii ya FIU, yaani *Financial Intelligence Unit.* Kulikuwa na malalamiko kwamba labda kamati hii haina uwakilishi kutoka Zanzibar, haina sura ya Kimuungano. Inawezekana kwa sababu hii dhana ni mpya hata kule Tanzania Bara hii dhana ni mpya na imewachukua kazi sana kuweza kuitengeneza.

Mhe. Spika, naomba nimuhakikishie Mhe. Salmin Awadh kwamba kwanza hii sio kamati isipokuwa ni *commission*, yaani ni kama *department* ambayo inajitegemea, na iliyonayo ni kamishna halafu na *staff* wengine pale ndani na kazi yake kubwa kama inavyoitwa ni *Financial Intelligence,* yaani kufanya uchunguzi wa mwenendo wa hizi fedha haramu na zaidi kufanya uchunguzi wa hizi zinazoitwa *suspicious transaction.* Kwanza kuna makubaliano ya kwamba inapotokea nafasi yoyote inatangazwa, watu wanaomba na baadae wanaajiriwa kwa mujibu wa utaalamu wao. Lakini sasa hivi kulikuwa kuna tatizo la uwezo wa hata serikali yenyewe na ni moja katika mambo ambayo yalilalamikiwa kuwa ilikuwa haijaiwezesha sana, maana ilikuwa na mfanyakazi mmoja kamishna na mfanyakazi mmoja mwengine.

Mhe. Spika, kwanza yenyewe ni hali katika kuianzisha, lakini inachofanya kazi yake ni kusikiliza tu yaani ni chombo cha upelelezi kama kilivyokuwa chombo cha polisi. Kwa

hivyo, zinapotokea nafasi tuwashajihishe ndugu zetu na jamaa zetu waombe wa hapa Zanzibar, kwa sababu hii ni fursa ambayo wanaweza kuitumia katika ajira. Pengine hapo mbele zitakapotoka hizi nafasi basi ni vizuri tuwashajihishe watu wetu waweze kupata. Moja katika jambo ambalo nimefanya na limewawezesha na Zanzibar.

Kwa mfano sisi hatukuwa na mtu hata mmoja ambaye anafanya kazi ya *evaluation*, lakini baada ya mazungumzo kuna mwanasheria wetu mmoja kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, ambaye aliteuliwa kufanyakazi za *evaluation* na wanatembea katika nchi mbali mbali za SADEC kwa ajili ya kufanya kazi hizi, kuzitizama nchi nyengine kama zinatimiza vigezo vya kimataifa katika usimamizi wa sheria hii. Kwa hivyo, mimi nadhani kwamba sura ya Kimuungano kadiri siku zinavyokwenda ndivyo tunavyojaribu kuijenga kutokana na mambo mbali mbali ambayo yanajitokeza katika kitengo hiki. Kwa hivyo, kwa kweli hii sio kamati isipokuwa ni *department* ambayo ni huru na inafanyakazi za kitaalamu.

Mhe. Spika, mimi naomba mtuamini kwamba hiyo kuangalia maslahi ya Zanzibar katika suala hili ni jambo ambalo tunalisimamia kwa makini sana na ndio maana hata ilipopitishwa hii sheria tukasema hapana, jamani haya sio yakwenu, yaliyokuwa ya pamoja tutafanya kwa pamoja. Kwa hivyo, hilo mimi nawaomba Waheshimiwa Wajumbe niwatowe wasi wasi kwamba suala hilo tunalizingatia kwa makini sana na tunashirikiana na wenzetu kwa karibu vile vile.

Mwisho Mhe. Spika, naomba niwashukuru tena Waheshimiwa Wajumbe kwa michango na maelezo mbali mbali ambayo wameyatoa. Yale ya kuyafanyiakazi tutayafanyia kazi na yale ya kurekebisha basi tutayarekebisha. Mwisho niwaombe Waheshimiwa Wajumbe, tuipitishe sheria hii ili tuweze kupata nguvu na tuweze kupata heshima, maana tulipokataa ile ya Muungano tulisemwa maneno mengi na tukaonekana hatuna nia ya dhati. Sasa hivi tumejijengea heshima kwamba hatukuwa na nia hiyo na sisi tumekuwa mbele zaidi katika kufanya marekebisho, nadhani wenzetu watapeleka marekebisho katika vikao vya huko mbele vya Bunge. Lakini sisi tumeonesha kuwa hatuna wasi wasi kwenye suala hili na nia yetu ilikuwa ni ya dhati kabisa, lakini tulitaka katiba yetu ya nchi yetu ya Muungano ifuatwe, hatukuwa na nia ya kukwamisha wala hatukuwa na nia ya kwamba sisi tunapenda fedha haramu.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe, mimi nawaomba sana tuipitishe sheria hii ili tuzipe taasisi zetu uwezo wa kufanya kazi zaidi. Nawashukuru sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, baada ya maelezo na ufafanuzi huo ambao naamini Waheshimiwa Wajumbe wamenifahamu naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza zima, ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Baadhi ya Sheria na Kuweka Masharti Bora Ndani yake

SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI

Kifungu cha 1 Jina Fupi na Kuanza Kutumika.

SEHEMU YA PILI

MAREKEBISHO YA SHERIA YA KUZUIA MADAWA YA KULEVYA NAM. 9 YA MWAKA 2009

Kifungu cha 2 Kusomwa.

Kifungu cha 3 Marekebisho ya Kifungu cha 1 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 4 Marekebisho ya Kifungu cha 2 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 5 Marekebisho ya Kifungu cha 4 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 6 Kuongezwa kwa Vifungu vipya vya 4(a), 4(b) na 4(c) pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 7 Marekebisho ya Kifungu cha 5 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 8 Marekebisho ya Kifungu cha 7.

Kifungu cha 9 Marekebisho ya Kifungu cha 10.

Kifungu cha 10 Marekebisho ya Kifungu cha 15 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 11 Marekebisho ya Kifungu cha 16.

Kifungu cha 12 Marekebisho ya Kifungu cha 18.

Kifungu cha 13 Marekebisho ya Kifungu cha 19 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 14 Marekebisho ya Kifungu cha 22 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 15 Marekebisho ya Kifungu cha 23.

Kifungu cha 16 Kuongezwa Kifungu kipya cha 32(a).

Kifungu cha 17 Kuongezwa kwa Kifungu kipya cha 33(a).

Kifungu cha 18 Kufutwa kwa Kifungu cha 48 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 19 Marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Nam.7 ya mwaka 2004 pamoja na marekebisho yake.

SEHEMU YA TATU

MAREKEBISHO YA SHERIA YA KUDHIBITI USAFIRISHAJI WA FEDHA HARAMU NA MAPATO YA UHALIFU NAM. 10 YA MWAKA 2009

Kifungu cha 20 Kusomwa pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 21 Marekebisho ya Kifungu cha 2 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 22 Kuongezwa Vifungu vipya vya 6(a) na 6(b) pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 23 Kuongezwa Kifungu kipya cha 9(a) pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 24 Marekebisho ya Kifungu cha 10 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 25 Marekebisho ya Kifungu cha 11.

Kifungu cha 26 Marekebisho ya Kifungu cha 12

Kifungu cha 27 Kuongezwa kwa Kifungu kipya cha 14(a) pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 28 Marekebisho ya Kifungu cha 15.

Kifungu cha 29 Marekebisho ya Kifungu cha 16 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 30 Marekebisho ya Kifungu cha 17.

Kifungu cha 31 Kuongezwa kwa Kifungu kipya cha 17(a) pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 32	Marekebisho ya Kifungu cha 18.
Kifungu cha 33	Kuongezwa kwa Kifungu kipya cha 18(a) pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 34	Marekebisho ya Kifungu cha 23.
Kifungu cha 35	Kuongezwa Vifungu vipya vya 81(a) na 81(b) pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 36	Marekebisho ya Kifungu cha 87 pamoja na marekebisho yake.

(Hapa Baraza lilirudia)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, ilivyokuwa kamati ya Baraza zima imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali, pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na swada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbali Mbali ya Mwaka 2011

(Mswada kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali ya Mwaka 2011, kusomwa kwa mara ya pili. Naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Katibu: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Baadhi ya Sheria na Kuweka Masharti Bora Ndani yake. Sasa umepitishwa rasmi na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

SHUKRANI/ MATANGAZO

Mhe. Spika: Kwanza Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru sana kwa mashirikiano makubwa mliotupa kuweza kuendesha kikao hiki na kuifanya shughuli hiyo kwa ufanisi mkubwa. Nimeambiwa kwamba hapa ndio mwisho wa shughuli zetu kwa leo. Lakini kabla ya kuahirisha kikao chetu, naomba niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wanachama wa UWAWAZA wanatakiwa ndani ya ukumbi kutakuwa na mkutano mdogo na baadae wakimaliza na wao watakuwa wamemaliza shughuli zao.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya shughuli hiyo basi tusitishe shughuli zetu hizi kwa kuwa hakuna shughuli nyengine ya kuja jioni na kwa maana hiyo niahirishe kikao hiki mpaka kesho tarehe 26/10/2011 saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 5:25 asubuhi Baraza liliahirishwa hadi tarehe 26/10/2011
saa 3:00 barabara za asubuhi)